**Wadau** wasema kufutwa tozo miamala simu kutaleta nafuu

UKURASA 3



**Dereva** aliyesababisha ajali vifo 10 akiwamo mwandishi wa Nipashe kortini

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Juni 23, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581350

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




UENDESHAJI BANDARI

# Wabunge wataka Rais Samia asirudi nyuma



"Niiombe serikali ikubali ushauri, isikilize wananchi, lakini wakati mwingine isikubali kuyumbishwa na watu wenye nia zao za kuitaka nchi yetu isiendelee kiuchumi.

**JERRY SLAA**



"Profesa Tibaijuka aiache serikali inayoongozwa na mwanamama mwenziwe ifanye kazi yake.

**SUBIRA MGALU**



"Maneno haya yangekuwa yanatoboa mwili wako, leo Waziri Mwigulu ungekuwa umejaa viraka na bandeji mwili mzima. Sasa kuwa na ngozi ngumu tu kujenga imani halafu baadaye unatoboa.

**HAMIS TABASAMU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### MIILI YA WATU 3 AJALI YA BASI YATAMBULIWA



MIILI ya watu watatu kati ya saba akiwamo dereva Kelvin Sanga (34), waliofariki dunia kwenye ajali ya basi la Kampuni ya New Force...

## Mama, watoto watatu, wateketea kwa moto wakiwa wamelala

UKURASA 3



## Spika atoa msimamo sakata bei ya mahindi

UKURASA 2

**MICHEZO** KAKOLANYA AAGA SIMBA, NYONI NAYE UK.24

**KATUNI** UK.6

# Wabunge wataka Rais Samia asirudi nyuma

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

WABUNGE wameishauri serikali kutosikiliza maneno ya watu mtandaoni kuhusu ushirikiano wa Serikali za Tanzania na Dubai katika makubaliano ya uwekezaji kwenye bandari zilizopo nchini (IGA) kwa kuwa wanaofanya hivyo hawaitakii nchi mema.

Pia, wameitaka serikali kuharakisha kusaini mikataba inayohusiana na suala hilo, ili bandari iwe sehemu ya kuchangia Pato la Taifa na kuletea maendeleo.

Waliyasema hayo jana wakati wanachangia hoja ya Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2023/24.

Mbunge wa Jimbo la Ukonga (CCM), Jerry Silaa, aliishauri serikali isikubali maneno ya watu wasiotaka iendelee kiuchumi ambao wanapinga uamuzi wake wa kushirikisha sekta binafsi kwenye maendeleo, ikiwamo ushirikiano ilioyongia na Serikali ya Dubai kuhusu uwekezaji kwenye bandari nchini.

Alifafanua kuwa IGA siyo mkataba wa utekelezaji bali ni makubaliano baina ya Serikali ya Tanzania na Dubai kuhusu uwekezaji utakaofanyika kwenye bandari zilizopo katika nchi hiyo na kwamba mikataba ya kwenda kutekeleza miradi bado haijaingiwa.

Silaa alisema ushirikiano huo utaongeza ufanisi wa bandari na kufikia malengo ya serikali ya kukuza uchumi wa nchi kwa kuongeza forodha na kuboresha sekta za uchumi ikiwamo kilimo.

"Niiombe serikali ikubali ushauri, isikilize wananchi, lakini wakati mwingine isikubali kuyumbishwa na watu wenye nia zao za kuitaka nchi yetu isiendelee kiuchumi, ikubaliane na hoja za msingi za kutetea taifa letu, tuwe na uwekezaji na kushirikisha sekta binafsi katika ameneo ambayo wenzetu wamebobea," alisisitiza.

Kadhalika, alisema serikali haiwezi kupiga hatua bila ushirikiano na sekta binafsi huku akitoa mfano wa moja ya mafanikio ya ushirikishwaji wa sekta hiyo kuwa ni Benki ya NMB ambayo hivi karibuni serikali imevuna gawiwo la Sh. bilioni 45.5 na kodi ya Sh. bilioni 453.

Aidha, Mbunge huyo aliishukuru serikali kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ikiwamo ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, ambalo utekelezaji wake umefikia asilimia 96, ujenzi wa reli za umeme na adaraja la Kigogo Busisi, mradi wa mwezndo kasi awamu ya tatu, Gongo lamboto -Kariakoo.

Mbunge wa Viti maalum Mkoa wa Pwani (CCM), Subira Mgalu, aliishauri serikali kuchukua hatua za haraka kuleta mikataba itakayotokana na IGA ili wawekezaji waje na bandari iwe na nafasi ya kuchangia katika pato la ndani la taifa na serikali ipunguze kukopa.

Kuhusu hoja ya kuitwa mbunge mmoja mmoja kupigia kura muswada huo iliyotolewa na mbunge mstaafu Prof. Anna Tibaijuka, alisema hauna mashiko kwa kuwa utaratibu huo unafanyika kwenye kupitisha bajeti ya serikali pekee, masuala mengine ni utaratibu wa kuhojiwa na walishafanya hivyo.

"Lakini nataka nimkumbushe Prof. Tibaijuka alipokuwa waziri 2013 aliwasilisha mpango wa kuifanya Kigamboni kuwa mji wa trilioni 11, haukufanikiwa na tulioupitisha kwa kura za kuhojiwa kwa hiyo aiache serikali inayoongozwa na mwanamama mwenzie (Rais Samia Suluhu Hassan) ifanye kazi yake," alisema.

Hivi karibuni, Prof. Tibaijuka akihojiwa na chombo kimoja cha habari, alikosoa utaratibu wa kura ya pamoja uliotumiwa na Bunge katika kupitisha Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Makubaliano Kati ya Tanzania na serikali ya Dubai kwenye ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa bandari Tanzania.

Aidha, aliwatoa hofu wananchi kuwa bandari haiwezi kuuzwa kwa serikali kugawana idadi ya gati na mwekezaji bali mbinu iliyotumika ni kushirikisha sekta binafsi katika kukuza utendaji kazi wa bandari na kukuza uchumi wa nchi.

Vile vile, alisema bajeti kuu imeonyesha dhamira ya serikali ya kurejesha uuzwaji wa bidhaa nje ya nchi kwa kutenga zaidi ya Sh. bilioni 800 wazalishaji wa mazao, ili kuliletea taifa fedha za kigeni na kukuza uchumi.

Pia, katika mapendekezo ya bajeti ya serikali inatarajia kukusanya Sh. trilioni 44, kati ya hizo Sh. trilioni 31 zitakusanywa kutoka mapato ya ndani na kwamba ni lazima serikali ishirikishe sekta binafsi katika uwekezaji.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa na kudai risiti wanapofanya ununuzi ili kuhakikisha kuwa wanalipa kodi na serikali isiendelee kuleta kodi mpya kwa kuwa inategemea pesa hizo kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mbunge wa Sengerema, Hamis Tabasamu, alimshauri Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba, kutokatishwa tamaa na maneno yanayozunguka mitandaoni na mitaani bali kuwa na imani jambo analolifanya litakwenda kuiletea mafanikio nchi.

"Kuna watu ni majemedari wa kupiga kelele kwenye mitandao na kila maeneo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, maneno haya yangekuwa yanatoboa mwili wako leo ungekuwa umejaa viraka na bandeji mwili mzima, kwa hiyo unachotakiwa sasa hivi ni kuwa na ngozi ngumu tu kujenga imani halafu baadaye unatoboa," alisema.

Alimmshauri waziri huyo kuwashirikisha wabunge wakati wa uandaaji wa bajeti hizo ili watoe ushauri wa vitu muhimu vya kuwapo na kutokuwapo kwa kuwa wao wanajua matatizo ya wananchi ambao wengi wao kukosa pesa ndiyo kunawafanya waitukane serikali kwenye mitandao.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson akionyesha tuzo ya utayarishaji bora wa mahesabu waliyopata Bunge ya mshindi wa tatu (3) wa taarifa bora ya hesabu za Mwaka 2021, wakati akiongoza kikao cha 53 cha Mkutano wa 11 wa Bunge la Bajeti jijini Dodoma jana. Tuzo hiyo, imetolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), wakati wa maadhimisho ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwa bodi hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## SAKATA BEI YA MAHINDI

# Spika atoa msimamo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SAKATA la bei ya mahindi limeibuka tena bungeni huku Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, akiwataka wakulima kuuza kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa bei elekezi iliyotangazwa na serikali na endapo hayatanunuliwa hoja hiyo itajadiliwa kwenye mhimili huo.

Bei hiyo ni Sh. 800 kwa kilo kwa maeneo ya makao makuu ya mikoa inayolima mahindi na Sh. 600 kwa maeneo ya wilaya zilizopo pembezoni.

Spika Tulia alitoa kauli hiyo jana baada ya serikali kutoa majibu ya hoja ya dharura ya Mbunge wa Mbozi (CCM) George Mwanisongole, aliyeomba shughuli za Bunge ziahirishwe ili kujadili jambo la dharura ambalo hivi karibuni serikali iliweka zuio la kuuza mahindi nje ya nchi.

Dk. Tulia alisema hoja ya mbunge ni kuhusu bei kushuka na wakulima kuathirika huku serikali ikisema imeipatia fedha NFRA kununua mahindi kwenye makao mkuu ya mikoa inayolima zao hilo na kuwataka wakulima wapeleke kuuza vituo vya NFRA ambavyo vina bei kubwa.

"Kwa hiyo wabunge tuwaambie wakulima wetu wasiuze mahindi kwa bei rahisi wakauze NFRA kwa kuwa fedha zipo, sasa wakipeleka kule kama wasipozikuta fedha ndiyo hoja irudi hapa bungeni kwamba mheshimiwa tumepeleka NFRA na hawajalipwa fedha zao."

"Sasa kama bei kubwa ipo NFRA na wanakwenda kununua kwa bei ya chini sidhani kama tunaweza kuijadili hapa kama hoja ya dharura. Mimi nitawapa nafasi kwasababu bado tupo hapa Dodoma leo hii waambieni watu wenu wakauze mahindi NFRA ambako bei ni kubwa na kukiwa na changamoto mtaileta hiyo hoja tutaijadili kwa ngazi hiyo," alisema.

Alisema wabunge wawape majibu wakulima kuwa mahindi yananunuliwa NFRA kulingana na eneo ambalo NFRA ipo.

Katika hoja yake Mwaisongole alisema; "Zuio hilo limesababisha bei ya mahindi kuporomoka kwa kiasi kikubwa Mbeya, Mbozi debe moja la mahindi linauzwa Sh. 7,000 na bei inazidi kushuka hii inavunja moyo wakulima ambao wamejitolea na matokeo yake sasa tunakwenda ambako gunia la mahindi linakwenda kuuzwa kwa Sh. 15,000."

Aliomba shughuli za Bunge ziahirishwe ili kuishauri serikali kuokoa bei ya mahindi inayoporomoka na kuwanusuru wakulima ambao wataingia kwenye umaskini mkubwa ambao watalazimika kuuza gunia 10 kununua mfuko mmoja mbolea.

Spika Tulia alitoa nafasi kwa serikali kutoa ufafanuzi na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema hakuna mfanyabiashara yeyote aliyefuata utaratibu uliowekwa ambaye amezuiliwa kupata kibali ya kusafirisha.

Alisema hadi juzi wizara imetoa vibali vya zaidi ya tani 20,000 za mahindi na tani 15,000 za unga wa mahindi.

"Kilichokatazwa na serikali ni mtu kutoka nje ya nchi kwenda shambani kupakia mazao, kwenda mpakani kumlipa dalali Sh. 800,000 kuvushiwa mazao kwenda nje, kitu kingine tulichokataza ni mfanyabiashara yeyote kufanya biashara ya mazao bila leseni ya biashara, cheti cha mlipakodi na nyaraka zingine kwa ajili ya kusafirisha mazao."

"Watanzania tuna utamaduni wa kutaka sekta hii ijiendeshe kiholela hatuwezi kuruhusu Spika, lakini kama Bunge lako linataka tuendeshe kinyume na utaratibu tulete sheria tufute sheria ya usalama wa chakula, tufute sheria inayotaka kuwa na leseni na sheria ya kutaka mfanyabiashara kuwa na TIN," alisema.

Alibainisha kuwa bei elekezi ya serikali ya mahindi ni Sh. 800 kwa Sumbawanga Mjini, Mbeya Mjini, Njombe Mjini na Sh. 600 katika wilaya zilizopo pembezoni.

"Hii ndiyo bei inayotumika na serikali imeipatia NFRA Sh. bilioni 320 na wameanza kufungua vituo niwatake wakulima wa nchi nzima hatujazuia usafirishaji bali tunachozuia mfumo wa ununuzi na uuzaji kwa wafanyabiashara wa nje ya nchini, waje ndani ya nchi na asajili kampuni kwa mujibu wa sheria au anunue mazao kupitia kampuni za watanzania aingie nao mikataba," alisema.

Alisema, haiwezekani kusafirisha tani 500,000 hadi 700,000 na fedha zake hazionekani kwenye mfumo wa kiuchumi wa nchi.

# Mama, watoto watatu wateketea kwa moto

**Na Abdallah Bakari,**
MTWARA

WATU wanne wa familia moja katika Kijiji cha Luagala, wilayani Tandahimba, mkoani Mtwara, wamefariki dunia baada ya nyumba waliyokuwa wamelala kuteketea kwa moto.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kijijini hapo zilizothibitishwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mtwara, ACP Nicodemus Katembo, tukio hilo lilitokea Juni 21, mwaka huu, majira ya saa nne usiku.

Alisema wanafamilia hao walikuwa wamelala kwenye nyumba iliyozekwa kwa nyasi ambayo ilishika moto na kuteketea.

Aliwataja waliofariki dunia kuwa ni mama wa familia Rehema Hamisi (40), wanawe Adhiru Bakari (12) mwanafunzi wa darasa la tatu, Imran Shadil (3) na mtoto wa dada yake, Muba Salum (15).

"Watoto watatu wote walifariki papo hapo na mama aliokolewa na kukimbizwa Hospitali ya Luagala, lakini alifariki muda mfupi baadaye," alisema Katembo.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, chanzo cha ajali hiyo ni moto uliokuwa umewashwa ndani ya nyumba hiyo kwa ajili ya kupikia na kuachwa bila kuzimwa na kushika nyasi zilizoteketeza nyumba hiyo.

"Daktari amefanya uchunguzi wa miili ya marehemu na kubaini kuwa chanzo cha vifo vyao ni kukosa hewa na kuungua sehemu kubwa ya miili yao," alisema.

Alisema miili hiyo imekabidhiwa kwa ndugu wa marehemu kwa ajili ya mazishi.




Mufti Mkuu wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zubeir akizungumza wakati wa hafla ya kutimiza miaka minane ya uongozi wake tangu achaguliwe na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Kinondoni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Miili ya watu 3 ajali ya basi yatambuliwa

**Na Elizabeth John**, NJOMBE

MIILI ya watu watatu kati ya saba akiwamo dereva Kelvin Sanga (34), waliofariki dunia kwenye ajali ya basi la Kampuni ya New Force yenye namba za usajili T173 DZU, katika Kijiji cha Igando, Kata ya Kidugala, wilayani Wanging'ombe, mkoa wa Njombe imetambuliwa na kuchukuliwa na ndugu zao.

Ajali hiyo ilitokea Juni 21 majira ya saa 8.30 mchana, wakati basi hilo likitokea Dar es Salaam kuelekea mkoani Rukwa. Akizungumza jana na Nipashe kwa njia ya simu, Mganga Mfawidhi wa Hopitali ya Lutheran Ilembula, Dk. Pangamawe Kidenya, alisema majeruhi wanne wamepelekwa Hospitali ya Rufani mkoani Mbeya.

"Majeruhi 37 wanaendelea vizuri tupo kwenye harakati za kuwaruhusu waende nyumbani, lakini juzi (jana) tumewaruhusu saba waende nyumbani," alisema Kidenya.

Alisema, majeruhi wengi wameumia sehemu za mikononi, kichwani na miguuni, wengine walivunjika mikono, miguu na kichwani.

Awali, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, John Imori, akizungumza na waandishi wa habari, alisema basi hilo lilikuwa limebeba abiria 51 na kati ya waliojeruhiwa wanaume ni 21 na wanawake 27.

"Chanzo cha ajali ni hili basi la New Force lilikuwa likitokea jijini Dar es Salaam kwenda mkoani Rukwa Sumbawanga lilipofika hapa Igando kuna sehemu ya daraja likawa linataka ku 'ovartake' (kulipita) lori likapoteza uelekeo likagonga daraja likaingia mtaroni, ajali hii imesababisha vifo saba kati yao wanawake wanne na wanaume watatu," alisema Kamanda Imori.

# Wadau wasema kuondolewa tozo miamala ya simu kutaleta unafuu

**Na Romana Mallya**

WACHUMI, wanasiasa na wananchi wametofautiana kuhusu mapendekezo ongezeko la viwango vya kodi ya majengo huku hatua ya kufutwa kwa tozo za muda wa maongezi na miamala wakiitaja ni njia ya kuleta ahueni kwa Watanzania.

Juzi, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aliwasilisha bungeni jijiji Dodoma Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2023, unaopendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kieletroniki, Sura ya 306 kwa kufuta kifungu cha 164A.

Muswada huo unalenga kufuta tozo ya muda wa maongezi kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji na kufutwa tozo ya miamala ya kuhamisha fedha kieletroniki. Kuongeza viwango vya kodi ya majengo kutoka Sh 12,000 hadi Sh. 18,000 kwa yasiyo ya ghorofa na kutoka Sh. 60,000 kwenda Sh. 90,000 kwa kila sakafu ya ghorofa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini nchini (REPOA), Dk. Donald Mmari, akitoa maoni kuhusu tozo za muda wa maongezi na miamala, alisema idadi ya Watanzania wanaotumia huduma za mawasiliano na miamala ni wengi na wenye vipato tofauti wakiwano wa vipato vya chini.

"Kuondolewa kwa tozo ya muda wa maongezi kwa kila laini, kufuta tozo ya miamala ya kuhamisha fedha kieletronini kutasaidia watumiaji kupata ahueni," alisema.

Dk. Mmari alisema serikali inahitaji fedha hivyo, vyanzo vingine vimebuniwa ikiwamo kuongeza viwango vya kodi kwenye majengo. Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, alisema muswada huo ukipitishwa na kuwa sheria utachochea kasi ya ujasiriamali kupitia miamala ya simu na kuleta nafuu kubwa pia kwa matumizi ya kawaida ya simu.

"Hili litachangia sana kwenye ongezeko la Pato la Taifa kwa kuzingatia kasi ya mawasiliano na idadi kubwa ya watumiaji wa mitandao ya simu katika kuanzisha mazungumzo na kujadiliana juu ya biashara mpaka kufikia muafaka na hatimaye kufanikisha miamala ya kuuza na kununua," alisema.

Kuhusu ongezeko la kodi ya majengo, Prof. Lipumba alisema nyongeza ya asilimia 50 ni kubwa kwa kuanzia.

"Mabadiliko haya yakipitishwa yataathiri sana uwezo wa kujikimu na hata ujasiriamali na uwekezaji wa kiwango cha chini na cha kati. "Kama tulivyoongea kwenye uchambuzi wa Bajeti Kuu ya Serikali 2023/24, Watanzania wengi ni masikini. Watanzania hawa masikini ndio wapangaji wa majengo haya ama kwa ajili ya makazi au kwa ujasiriamali wa kawaida," alisema.

Prof. Lipumba alisema kupitishwa kwa sheria hiyo kutasababisha wapangaji wengi kuachia majengo ya ofisi na kuleta ongezeko la machinga mitaani na hatimaye kupunguza makusanyo rasmi ya kodi.

"CUF tunapendekeza kodi isiongezeke kwa zaidi ya asilimia 20 na serikali iandae mazingira yatakayofanya wajasiriamali na wafanyabiashara wengi zaidi kulipa kodi katika mazingira na viwango rafiki," alisema.

Mchumi Mbobezi, Prof. Samwel Wangwe, alisema kufutwa kwa tozo ni jambo zuri na litahamasisha uchumi wa kidigitali.

Kuhusu ongezeko la kodi ya majengo aliipongeza serikali kwa kuwa ni njia nzuri ya serikali ya kupanua wigo wa walipa kodi.

Mkazi wa Temeke Sterio, mkoani Dar es Salaam, Joseph Peter, alisema kuondolewa kwa tozo kutaongeza matumizi ya huduma za kieletroniki.

Kuongezeka kodi ya majengo, alisema ni sawa kwa sababu watu watapata faida kubwa, itapandisha thamani ya nyumba na ardhi na kuongeza makusanyo serikalini.

## CRDB yaahidi mikopo zaidi, ikifungua tawi jipya Igunga

**Na Mwandishi Wetu,** IGUNGA

BAADA ya kukopesha Sh. bilioni 129 katika sekta ya kilimo hasa cha tumbaku mkoani Tabora kuanzia Januari mpaka sasa, Benki ya CRDB imeahidi kufungua fursa zaidi kwa wananchi wilayani Igunga.

Ahadi hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Mikopo wa Benki ya CRDB, Xavery Makwi, wakati wa ufunguzi wa tawi la benki hiyo wilayani Igunga.

Makwi alisema kwa uzinduzi huo, wanafikisha matawi 253, hivyo kuifanya taasisi hiyo kuongoza kwa mtandao mpana zaidi nchini.

"Kuanzia Januari mpaka sasa, benki yetu imeshakopesha zaidi ya Sh. bilioni 129, sehemu kubwa ikielekezwa kwenye kilimo na biashara ya tumbaku. Tawi hili litakuwa lango la fursa za kiuchumi kwa wana Igunga kuimarisha kipato chao," alisema Makwi.

Benki ya CRDB ilianzishwa mwaka 1996 ikiwa na matawi 19 na kwa muda mrefu mkoani Tabora ilikuwa na matawi matano katika wilaya za Nzega, Sikonge, Tabora Mjini, Urambo na Kaliua.

Hata hivyo, wananchi, wafanyabiashara na wawekezaji walizitumia pia huduma zinazotolewa na mawakala zaidi ya 300 waliopo wakiwamo takriban 70 wa wilayani Igunga.

Makwi alisema benki yao inatoa mikopo ya aina tofauti kulingana na mahitaji ya mteja, akiitaja ya uwekezaji na uendeshaji biashara, mikopo binafsi kwa ajili ya wafanyakazi, mikopo kwa wajasiriamali, mikopo ya vikundi, wanafunzi na wastaafu.

Akilizindua tawi hilo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Batilda Burian, alisema Wilaya ya Igunga iliyoanzishwa Julai 1975 ikimegwa kutoka Wilaya ya Nzega inazo fursa nyingi za kiuchumi, hivyo kupatikana kwa huduma za uhakika za benki kutachochea maendeleo ya wananchi.

"Benki ya CRDB ndiyo inayoongoza kwa mtandao mpana zaidi nchini. Tawi hili tunalolizindua litazihudumia tarafa zote nne za Wilaya ya Igunga ambazo ni Igunga, Simbo, Manonga na Igurubi zenye kata 35 na vijiji 119.

Mkuu wa Mkoa alisema serikali imejitahidi kujenga vituo 55 vya afya wilayani humo vinavyotoa huduma za uhakika kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema, hivyo wakipata fedha za kuanzisha au kuendeleza biashara zao, maendeleo ya kiuchumi litakuwa jambo la uhakika.

"Mnayo Programu ya Imbeju inayowawezesha vijana na wanawake, halmashauri inashirikiana na vikundi 136 vya wanawake na vijana ambavyo vina nafasi kubwa ya kunufaika na programu hii inayotoa mtaji wezeshi. Iwapo fursa za Imbeju zitachangamkiwa na wana Igunga, hakika huu utakuwa mwaka unaoweka msingi wa mafanikio ya kiuchumi kwa wengi," alisisitiza.

CRDB ndio benki pekee ya kizalendo inayotoa huduma nje ya mipaka ya Tanzania ikiwa na matawi Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Baada ya uzoefu wa takriban miaka 15 ya kutoa huduma za bima, mwezi uliopita benki hiyo ilipewa leseni ya kuanzisha kampuni yake ya bima iitwayo CRDB Insurance Company Limited ambayo huduma zake Makwi alisema zinapatikana kwenye matawi yote ya benki hiyo.




Mhifadhi wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA), Kanda ya Dar es Salaam, Msafiri Kasara akitoa mada ya jitihada za kukuza utalii na kukabili ujangili, kwa waandishi wa habari za utalii na uhifadhi kwenye mafunzo yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET), jijini Dar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BoT yapiga marufuku taasisi kutoa mikopo bila leseni

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imepiga marufuku wanaojihusisha na biashara ndogo za huduma za fedha, ikiwamo kukopesha bila kuwa na leseni.

Taarifa ya Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, ilisema wamebaini kuwapo kwa baadhi ya taasisi, kampuni na watu binafsi wanaojihusisha na biashara ya kutoa mikopo bila kuwa na leseni jambo ambalo ni kinyume na kifungu cha 16 (1) cha sheria ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2018.

Alisema kwa taasisi, kampuni au mtu atakayebainika kujihusisha na biashara hiyo kinyume cha sheria atachukuliwa hatua kali, ikiwamo faini au kufungwa jela.

"Taasisi, kampuni na mtu binafsi wasio na na leseni hawaruhusiwi kufanya biashara ya kukopesha, kifungu cha 16(2) (a) cha sheria ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2018, hatua zitakazochukuliwa kwa ukiukwaji wa sheria hiyo ni pamoja na faini isiyopungua Sh.milioni 20 au kifungo cha muda usiopungua miaka miwili."

"Benki Kuu inawakumbusha watoa huduma ndogo za fedha waliokwisha kupata leseni kufuata sheria, kanuni na miongozo inayotolewa ikiwamo kuwapa wakopaji mikataba, kuonyesha riba ya mikopo kama ilivyopitishwa kwenye sera ya mkopo, gharama nyingine zote wanazotoza na riba kukokotolewa kwa mwezi na siyo kwa siku."

Aliwataka wananchi kuepuka kukopa au kufanya biashara na taasisi, kampuni au watu binafsi wasio na leseni ya utoaji wa huduma hiyo.

## Chongolo ataka serikali kutangaza zabuni ukarabati skimu umwagiliaji

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameiagiza serikali kupitia Tume ya Umwagiliaji ifikapo Julai Mosi, mwaka huu kutangaza zabuni za ukarabati wa skimu za umwagiliaji 22 zilizopo nchini.

Alitoa agizo hilo wakati alipokuwa katika mkutano wa Shina namba 18, tawi la CCM Bahi Sokoni, Wilaya ya Bahi, mkoani hapa juzi.

Aliagiza Wizara ya Kilimo, ukarabati na ujenzi wa skimu hizo uanze haraka na wananchi waanze uzalishaji wa mazao.

"Maelekezo yangu kwa serikali kuhakikisha kuwa kuanzia Julai Mosi, mwaka huu, tangazeni tenda za skimu zote zinazohitaji ukarabati, kama upembuzi yakinifu umeshakamilika tangazeni zabuni ili ukarabati na ujenzi ufanyike," alisema.

Kadhalika, alisema ucheleweshaji wa miradi hiyo inasababisha kukwama kutokana na ongezeko la gharama za vifaa na ufundi.

Akiwa kwenye mkutano huo, Chongolo alipokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa eneo hilo ya miundombinu ya skimu ya umwagiliaji kuchakaa na kushindwa kuzalisha mazao ya kutosha.

Mmoja wa wakazi hao, Isaya Daudi alisema, miundombinu ya skimu hiyo ilifanyiwa ukarabati wa mwisho mwaka 1998 na kuiomba serikali kuwasaidia kufanya ukarabati mwingine.

"Uzalishaji wa mpunga katika eneo letu umeshuka tulitakiwa kulisha mkoa mzima wa Dodoma, lakini sasa tunapata mazao kidogo kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu hiyo," alisema.

Daudi alisema kuwa umwagiliaji Bahi, unavikundi sita vinavyojumuisha Mtajira, Uhelela, Bahi Sokoni, Nguvu Mali na Mtazamo, vyote vinajihusisha na kilimo cha mpunga.

Kadhalika, kuna wakulima wengine mmoja moja ambao wanajishughulisha na kilimo hicho, lakini tatizo la uchakavu huo wamekwama kuongeza mashamba na wengine wameshindwa kuyaendeleza.

## HABARI KITAIFA

MAUAJI DADA WA BILIONEA MSUYA

# Wakili atupia lawama upande wa mashtaka

**Na Grace Gurisha**

WAKILI wa Utetezi, Peter Kibatala amedai mahakamani kuwa upande wa mashtaka haujatenda haki katika kesi ya mauji ya mdogo wa marehemu Erasto Msuya, maarufu kama Bilionea Msuya, Aneth Msuya kwa kushindwa kupeleka mashahidi kwa siku mbili mfululizo.

Aidha, amedai kuwa kilichotokea siyo haki kwao, kwa washtakiwa, ndugu na jamaa waliotoka mikoani kuja kusikiliza kesi, mahakamani na hata kwa Mungu pia, kwa sababu wapo mahabusu miaka saba sasa.

Kibatala alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki, Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, wakati kesi hiyo ya mauaji inayomkabili aliyekuwa mke wa bilionea huyo, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela, ilipokuja kwa ajili ya kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka.

Wakili Kibatala alifikia hatua hiyo, baada ya Wakili wa Serikali Mwandamizi Yasinta Peter, kuomba ahirisho la siku mbili mfulululizo kwa sababu mashahidi waliowaandaa kupata dharura huku akitoa wito wa mahakama kuonesha udharura kwa mashahidi hao wawili.

Kibatala, baada ya kukagua wito huo, alidai; "Tunasikitika kwa kilichotokea hii siyo haki kwetu, kwa wateja waliokaa mahabusu, kwako kwa Msajili na hata kwa Mungu."

"Hizi session (vikao vya mahakama) zinapatikana kwa tabu sana mara ya mwisho ilikuwa Machi, 2022 imepita miezi 15 ndiyo tumepangiwa tena Juni 12, halafu leo haya ndiyo yanatokea," alidai Kibatala.

"Mahakama inapotoa samansi tayari unakuwa umeshajipanga kwa sababu kesi inasikilizwa mfululizo, halafu ukiangalia hizi samansi zimesainiwa leo Juni 22, 2023, kinachoonekana hiki nini?" Alihoji Kibatala.

Awali, Peter alidai kuwa kesi ilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa, lakini upande wa mashtaka kwa jana, hawakuwa na shahidi na siku ya leo hawatakuwa na shahidi pia.

Alidai kuwa walitarajia kuwa na shahidi Dk. Fidelis Segumba, lakini walirudishiwa wito wa mahakama kuwa anaumwa na yuko nchini India kwenye matibabu.

Pia kwa leo walimuandaa Polisi, Mwaka lakini wamejulishwa kuwa amejifungua kwa operesheni tangu Juni 19, 2023.

"Tungeweza kuwaleta mashahidi wengine, lakini kwa kuwa kesi hii ni ya muda mrefu mashahidi wengi wako sehemu mbalimbali mikoani na jana wasingeweza kufanya lolote baada ya kuwakosa waliokuwa wanawatarajia," alidai.

"Upande wa mashitaka hauna lengo la kukwamisha kuendelea kusikilizwa kwa kesi hii, hivyo tunafanya kila namna ili iendelee kusikilizwa kama ilivyopangwa," alidai Peter.

Aliomba ahirisho chini ya kifungu cha 284(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kutokana na sababu walizoifahamisha mahakama.

Pia, aliomba kuwasilisha mahakamani samansi zilizokuwa zimepelekwa kwa mashahidi hao ili kuunga mkono hoja walizoziwasilisha.

Akijibu kuhusu samansi, Peter alidai kuwa wapo wengi, kuna mwenzake ndiyo alikuwa anashughulikia.

Jaji: Kama samansi haijasainiwa inawezaje kuwa served (kutolewa)?

"Aliyezushughulikia hayuko hapa lakini lengo lilikuwa ni kuweka uharaka ili mashahidi wapatikane," alidai.

Katika uamuzi wake, Jaji Kakolaki alisema mahakama imeangalia samansi ni kweli imesaniwa (jana) na imekuwa endorsed (kupitishwa) jana na hii inaleta mkanganyiko.

"Ifahamike msimamo wa mahakama ni kwamba haki haipaswi kucheleweshwa, pale kesi inapopangwa inatakiwa isikilizwe kama ilivyopangwa. Nawakumbusha upande wa Jamhuri kuwa na jukumu la kuleta mashahidi bila kukosa ili shauri lisikilizwe kwa muda uliopangwa," alisema.

Alisema kama Kibatala alivyosema hili shauri ni la muda mrefu washtakiwa wamekaa ndani miaka saba, lakini kwa kuwa maombi haya ya ahirisho kwa kutokuwapo mashahidi yameletwa kwa mara ya kwanza, mahakama inayakubali.

Alisema shauri linaahirishwa hadi Juni 26, mwaka huu.




Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa (kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Lilian Mbassy baada ya kufungua mkutano wa wadau wa benki hiyo, Kanda ya Arusha jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi kwa Umma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dereva mbaroni ajali iliyoua 10 akiwamo mwandishi wa Nipashe

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

DEREVA Faraja Manyama (52), aliyesababisha ajali na kuua watu 10 akiwamo mwandishi wa habari wa gazeti hili Machi 7, mwaka huu na kukimbia, ametiwa mbaroni na kufikishwa Mahakama ya Wilaya ya Geita.

Katika mahakama hiyo amepandishwa kizimbani kwa mashtaka 67 yakiwamo ya kuendesha gari bovu lenye namba za usajili T 922 ADC aina ya Scania katika barabara ya Sengerema-Kasamwa, ajali ambayo pia ilisababisha majeruhi 53.

Waliofariki katika ajali hiyo Raulesia Peter, Christina Pastory, Nyabutwema Nyamwelo, George Peter, Elizabeth Elkana, Crispin Emmanuel, aliyekuwa mwandishi wa gazeti hili mkoani Mwanza, Richard Makore, Nyabuso Kalungu, Julius Masolwa na Abdiel Twenye.

Manyama alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samweli Maweda, hata hivyo alikana makosa yote na yuko nje kwa dhamana ya wadhamini wawili ambao walitoa barua za utambulisho kutoka kwa mtendaji wa kata.

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Scolastica Teffe, ulidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa. Kesi hiyo iliahirishwa hadi Julai 11, mwaka huu.

Awali, Wakili wa Serikali, Teffe alidai tukio hilo lilitokea Machi 7, mwaka huu katika Kijiji cha Mwilima barabara ya Sengerema-Kasamwa, Mkoa wa Geita.

Alidai kuwa mtuhumiwa huyo anakabiliwa na makosa mengine ya kuendesha gari bovu kwa uzembe.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mkuu**

**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mapendekezo Muswada Sheria ya Fedha wasubiriwa kwa hamu

**KUWASILISHWA** kwa Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2023 bungeni, ambao unapendekeza marekebisho katika baadhi ya vifungu ikiwamo cha kufuta tozo ya muda wa maongezi kwa laini za simu na kufutwa kwa tozo ya miamala ya kuhamisha fedha kielektroniki ili kuwaondolea wananchi mzigo wa tozo hizo, kumeleta matumaini kwa wananoumia kwa tozo hizo.

Waziri wa Fedha na Mipango, akiwasilisha Muswada huo bungeni, aliliambia Bunge kuwa mapendekezo mengine ni kuongezwa kwa tozo kwenye bidhaa mbalimbali.

Tozo za miamala ya simu ni kilio kilichokuwa kikitolewa na wananchi kila mara kutokana na viwango vya pesa wanavyokatwa wanapofanya miamala kwa njia ya simu.

Mwananchi inamlazimu kuwa na fedha ya ziada ya kutuma na kutolea anapotaka kumtumia mtu pesa kwa njia ya simu. Suala hili limekuwa likiwaumiza watu wengi na wengine kuona bora atumie nauli ya Sh. 1000 kumfikishia mtu wake pesa anayohitaji kuliko kutuma kwa njia ya simu ambayo ni rahisi zaidi.

Mapendekezo ya Muswada wa Sheria hiyo yakipitishwa yatatoa nafuu kubwa kwa wafanyabiashara na hata wasiokuwa wafanyabiashara kwa kuokoa makato waliyokuwa wakikatwa kupitia tozo za miamala.

Hata kampuni za simu ambazo zilikuwa zikilalamika kuyumba kiuchumi kutokana na tozo hizo zitapata faraja Muswada huo wa sheria utakapopitishwa.

Serikali ina njia nyingi za kukusanya kodi bila kumuumiza mtu wa chini ambaye kipato chake cha siku ni kidogo kwa kumudu kuiendesha familia.

Pia, ingeangalia kodi kwenye vifaa vya ujenzi vinavyozalishwa hapa nchini kupunguziwa ushuru ili viweze kutengeneza bidhaa watakazomudu Watanzania kuzinunua na kuwawezesha kuwa na makazi bora na ya kudumu.

Muswada huo pia unapendekeza kurekebishwa kwa kubadili utaratibu wa kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kutoka kila mwaka na kuwa kila baada ya miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2023/24.

Lengo la marekebisho hayo ni kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji. Kadhalika baadhi ya vifungu kwenye muswada huo vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuanzisha kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye magari ya abiria yanayotumia teknolojia ya kisasa yanayotumika zaidi ya miaka mitano tangu yalipotengenezwa ili kupunguza uingizaji wa magari chakavu na kulinda usalama wa abiria.

Pia, Muswada huo unapendekeza kurekebisha utaratibu wa ukadiriaji kodi ya mapato kwa walipa kodi binafsi ambao wanafanyabiashara ya usafirishaji wa abiria na mizigo na hawana wajibu wa kisheria wa kuwasilisha ritani za kodi.

Aidha, unapendekeza kufuta na kuweka utaratibu wa kukadiria kodi ya mapato kwa wasafirishaji wa abiria na mizigo kwa kutumia viwango elekezi vya kodi kwa kila gari kwa walipakodi binafsi ambao hawana wajibu kisheria kuwasilisha ritani za kodi.

Ni matarajio ya Watanzania wengi kuwa Muswada huo utakapopitishwa watapata ahueni kwa baadhi ya kodi zilizokuwa zikiwaumiza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Enyi vijana msibeze ushauri huu kukabiliana na sikoseli

Na Sabato Kasika

**JUNI** 19 ya kila mwaka, ni Siku ya Sikoseli Duniani kama ilivyoamriwa na Umoja wa Mataifa, katika mojawapo ya Malengo ya Milenia, ikiwa siku ya kutafakari na kuweka mikakati ya kukabiliana na ugonjwa huo.

Katika kukabiliana na ugonjwa huo serikali inafanya kila jitihada za kutoa elimu ya kutosha kwa jamii, ili kuongeza uelewa na pia kuboresha huduma za afya na matibabu yanayotolewa kwa watu wenye sikoseli.

Kwa mfano, katika maadhimisho ya mwaka huu, Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, anasema ugonjwa huo husababishwa na kurithi vinasaba kutoka kwa wazazi wote wawili, hivyo ili kupunguza kuenea kwake, vijana wanatakiwa kupima kabla ya kuanzisha uhusiano.

Sababu za maelekezo hayo ni kwamba, ugonjwa huo ni wa kurithi, hivyo ni wazi elimu hiyo ya kuwataka vijana kupima kwanza ni ya muhimu, ili kulinda afya za watoto watakaowazaa.

Ninaunga mkono ushauri huo wa waziri, kwani anaeleza kwamba takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 15 hadi 20 ya Watanzania wana vinasaba vya ugonjwa huo na wana uwezekano wa kupata watoto wenye sikoseli iwapo watakuwa na wenza wenye vinasaba vya ugonjwa huo. Ili kuchukua tahadhari, kunaweza kusaidia kupunguza idadi ya watoto wanaozaliwa wakiwa na ugonjwa huo, hasa kwa kuchunguza afya kabla ya kuingia katika ndoa au uhusiano.

Kwa mujibu wa waziri huyo, inakadiriwa kuwa kila mwaka, takriban watoto 11,000 huzaliwa wakiwa na ugonjwa wa sikoseli nchini, na kwamba Tanzania ni nchi ya tano duniani yenye wagonjwa wengi.

Tanzania inashika namba tano kwa watu wengi wenye ugonjwa huo, ikitanguliwa na Nigeria, India, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Angola, hivyo ni muhimu kupima vinasaba vya sikoseli kabla ya kuoana au kuanzisha familia.

Ikumbukwe, wataalam wa afya wanaeleza kuwa watoto wenye ugonjwa huo mara nyingi hupata maambukizi ya bakteria, maumivu kwenye mifupa (misuli) na kupungukiwa damu kila mara.

Hali hiyo inaelezwa kuwa inachangia kuathiri ukuaji wao na maendeleo yao shuleni, kwa kuwa wanashindwa kuhudhuria masomo mara kwa mara kutokana na kuumwa.

Si hapo tu, bali pia inaelezwa kuwa watoto wengi wanaozaliwa wakiwa na sikoseli wanafikia asilimia 70, huku watoto saba kati ya 100 hufariki dunia kabla ya kutimiza umri wa miaka mitano.

Kwa kuwa serikali imeshaweka wazi kwamba inaendelea kuboresha huduma za wagonjwa wa sikoseli kwa kuanzisha kliniki za ugonjwa huo katika hospitali za rufani za mikoa na baadhi ya hospitali za halmashauri na vituo vya afya, ni muhimu jamii ikachukua tahadhari.

Inafafanua kuwa mwelekeo wake, ni kuhakikisha kliniki za sikoseli zinaanzishwa katika hospitali zote za halmashauri na vituo vyote vya afya nchi nzima, ili kuimarisha huduma za ugunduzi wa mapema kwa watoto wachanga

Pia, kunatajwa kuwapo mkakati wa kutoa elimu kwa jamii kuhusu ugonjwa huo hasa kwa vijana kuhusu umuhimu wa kupima vinasaba vya sikoseli kabla ya kuoana au kuanzisha familia ili kuvunja mduara wa ugonjwa huo. Mkakati mwingine wa serikali, ni kuimarisha upatikanaji wa dawa ya Hydroxurea ambapo mwaka 2017 ni asilimia moja tu ya watoto wenye sikoseli ndio walipata dawa hiyo.

Aidha, kuna bima ya afya ya kiserikali, ambayo watoto wanaopata dawa ya hyrodroxurea, lengo likiwa ni kuhakikisha wote wenye sikoseli wanapata dawa hiyo bila kikwazo.

Mbali na hayo, serikali pia inasema ina mkakati wa kuimarisha huduma za kubadilisha kwa wagonjwa wa sikoseli wenye uhitaji, lakini pia kuanzisha huduma za kupandikiza uloto (bonne marrow transplant).

Hivyo, wakati serikali ikiwa na mikakati hiyo, ninadhani ni wajibu wazazi, walezi na vijana kuhakikisha wanakua na mchango mkubwa wa kudhibiti ugonjwa huo kwa kuzingatia maelekezo ya wizara.

## Tanzania inapoteza zaidi ya hekta 400,000 misitu kwa mwaka

**Na Joseph Mwendapole**

TANZANIA inapoteza hekta 469,000 za misitu kwa mwaka na kuchangia ongezeko la gesi joto la tani milioni 43.7.

Kwa sasa Tanzania inakadiriwa kuwa na hekta milioni 48.1 za misitu.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Kituo cha Kitaifa cha Kuratibu Kaboni, Profesa Eliakim Zahabu, wakati wa mkutano na wahariri wa vyombo vya habari.

Mkutano huo uliandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwaajili ya kutoa elimu kuhusu mabadiliko ya tabianchi na mchakato wa usimamizi wa biashara ya kaboni.

Alisema hali hiyo imekuwa ikisababisha kuzalishwa kwa gesi joto tani milioni 43.7 za kaboni na kama misitu itatunzwa inaweza kusababisha mabadiliko makubwa.

Alisema mwaka 1997 Umoja wa Mataifa (UN) ulianzisha Itifaki ya Kyoto ambayo nchi zilizoendelea zinatakiwa kupunguza uzalishaji wa gesijoto kwa asilimia tano.

Alitaja njia za kupunguza uzalishaji wa gesijoto kuwa ni ufanisi wa matumizi ya nishati, matumizi nishati mbadala na nishati endelevu.

Aidha, alisema nchi zilizoendelea zinaruhusiwa pia kuwekeza kwenye miradi ya kupunguza gesijoto kwa kufanya biashara ya kaboni kwenye nchi zinazoendelea.

Profesa Zahabu alitoa mifano ya aina ya miradi ya kaboni kuwa ni pamoja na nishati mbadala kama kutumia gesi badala ya kuni au mkaa, matumizi ya umeme wa maji, jua au upepo, kuongeza ufanisi wa matumizi ya nishati na matumizi ya nishati endelevu.

Alitaja mingine kuwa ni miradi ya menejimenti ya taka, miradi ya matumizi ya ardhi na misitu na kupanda misitu mipya ili kurudisha uoto wa asili.

Akizungumzia mapato yatokanayo na biashara ya kaboni, Profesa Zahabu alisema, Tanzania hadi mwisho wa 2021 imeshalipa Shilingi bilioni sita kwenye biashara hiyo.

Alitaja changamoto ya biashara ya kaboni kuwa ni mchakato mrefu na gharama kubwa za kuandaa miradi ya biashara hiyo, uhaba na ukosefu wa wataalam wa kuandaa miradi katika nchi zinazoendelea.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni uelewa mdogo katika biashara ya kaboni na mikakati ya kujenga uelewa inapaswa kuwa endelevu katika ngazi zote.

Profesa Zahabu alisema biashara ya kaboni inazidi kukua baada ya makubaliano ya Paris na uwapo wa mwongozo na kanuni za biashara ya kaboni nchini, utasaidia kuvutia uwekezaji katika biashara hiyo.

Alisema Tanzania ina nafasi kubwa ya kunufaika na biashara hiyo kiuchumi na utunzaji wa mazingira na inaweza kufikia hadi shilingi trilioni moja kwa mwaka.



Washiriki wa Semina ya Jinsia na Maendeleo (GDSS), inayoendeshwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), wakiwa katika vikundi vya majadiliano, Mabibo mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mbaroni kwa kunajisi, kuambukiza VVU

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MKAZI wa Mombasa Raha Kata ya Butundwe, Deogratius William (43) amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita kwa makosa ya kunajisi mtoto mwenye umri wa miaka 17 na kumwambukiza virusi vya Ukimwi kwa makusudi.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani juzi mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Nyakato Bigirwa na aliposomewa mashtaka alikana makosa yote mawili.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na mawakili wawili wa serikali, Godfrey Odupoy na Kabula Benjamin, walidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine ya kumsomea maelezo ya awali.

Hakimu Bigirwa alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Julai 5, mwaka huu.

Aidha, aliyataja masharti ya dhamana kwa mshtakiwa huyo kuwa na wadhamini wawili wenye barua ya utambulisho kutoka kwa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Shilingi milioni tano.

Akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, Godfrey Odupoy, alidai katika tarehe tofauti kati ya mwaka 2018 na 2023 katika maeneo ya Mombasa Raha, Kata ya Butundwe, Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimbaka mtoto mwenye umri wa miaka 17 na kumwambukiza virusi vya Ukimwi kwa makusudi kitendo ambacho ni kosa kisheria.

# Upelelezi wakwamisha kesi ya askari JWTZ

**Na Grace Gurisha**

UPELELEZI wa kesi inayomkabili Kapteni wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Exavery Mloso, kutoka kikosi jeshi 603 cha Anga, kituo cha Banana bado haujakamilika.

Inadaiwa kuwa Februari 11, 2023, mshtakiwa akiwa nchini India kwa makusudi kupitia mfumo wa kompyuta, aliingilia akaunti ya Instagram 'mamakajatz' kwa kubadili barua pepe ya mamajabackup@gmail.com kwenda zavobiashara@gmail.com huku akijua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Ilidaiwa na Wakili wa Serikali, Adolf Lema, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Rhoda Ngimilanga wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam, wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa.

Alidai upelelezi haukamilika na kuiomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa ambapo ilipangwa Julai 19, 2023.

Katika shitaka la pili ilidaiwa katika tarehe hizo, mshtakiwa huyo aliingilia mfumo wa data wa kompyuta wenye jina la Hashim Ally Mubi, Jerson Brown na Steven Magombeka kwa kubadilisha neno la siri akaunti ya Instagram kutoka mama2022 kwenda mamakaja 1321 huku akijua kufanya hivyo ni kosa la jinai.

Shtaka la tatu, alidaiwa kuwa katika tarehe hiyo, akiwa India, alizuia data za kompyuta kwa viongozi wa utawala wa akaunti ya Instagram ya mamajaztz ambao ni Hashim Ally Mubi, Jerson Brown na Steven Magombeka kwa kubadilisha neno la siri la akaunti hiyo kutoka mama2020 kwenda mamakaja 1321 huku akijua ni kosa.

Mshtakiwa huyo yupo nje kwa dhamana.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**






Dereva wa bodaboda Ambrose Kumbila akifurahia jambo na Meneja Masoko wa TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, Caroline Kakwezi (kulia) na Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa Vodacom Tanzania Plc, Harriet Lwakatare (wa pili kulia), baada ya kulipia mafuta kwa kutumia LIPA kwa M-Pesa, wakati wa uzinduzi rasmi wa huduma hiyo, jijini Dar es Salaam juzi, ikiwa ni ushirikiano baina ya huduma ya M-Pesa ya Vodacom na TotalEnergies, ili kuwawezesha wateja wa TotalEnergies kufanya malipo kwa masaa 24, kwenye vituo vyote vya kutolea huduma na maduka yote ya Bonjour nchini kote. Wengine ni Meneja Uendeshaji wa Mtandao wa TotalEnergies, Thomas Meitaron (wa tatu kushoto) na Mkurugenzi wa Udhibiti wa Hatari na Utii wa Sheria, Agapinus Tax (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shule zinazoweka wanafunzi chini ya darasa la 5 bweni kufutiwa usajili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imeliambia Bunge inafuatilia shule ambazo watoto chini ya darasa la tano wanasoma bweni kwa kuwa zinakiuka maelekezo na zitakazobainika zitafutiwa usajili.

Aidha, imesema kwa kushirikiana na wadau wa elimu, wizara inakamilisha kuandaa vigezo vitakavyotumiwa na Kamishna wa Elimu katika kutoa kibali maalumu.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Omary Kipanga, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Judith Kapinga.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kudhibiti watoto chini ya miaka saba kusoma shule za bweni.

Naibu Waziri Kipanga alisema serikali iliandaa mwongozo wa uanzishaji na usajili wa shule uliotolewa mwezi Novemba, 2020.

Alifafanua kuwa mwongozo huo umeelekeza bayana kuwa kibali cha kutoa huduma ya kulaza wanafunzi wa bweni kitatolewa kuanzia darasa la tano na kuendelea.

Aidha, huduma ya bweni itatolewa kwa kibali maalumu kwa wanafunzi wanaosoma chini ya darasa la tano.

Alifafanua kuwa pamoja na kutolewa kwa mwongozo huo pia, serikali imetoa Waraka wa Elimu Na. 2 wa mwaka 2023 unawaelekeza wamiliki wa shule wasiokuwa na kibali maalumu cha kutoa huduma ya bweni kwa wanafunzi walio chini ya darasa la tano wasiendelee kutoa huduma hiyo.

"Napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa serikali itaendelea kudhibiti tatizo la watoto chini ya darasa la tano kusoma shule za bweni kwa kuhakikisha kuwa inafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na shule itakayobainika kukiuka maelekezo hayo itachukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria ikiwamo kufutiwa usajili," alisema.

# Mashamba 40 ya mfano kahawa kufufuliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, amesema katika mikakati ya serikali ya kufufua zao la kahawa mashamba 40 ya mfano yamepangwa kuanzishwa kwenye wilaya 20 kwa mwaka 2023/24.

Pia, serikali imepanga kuratibu uzalishaji na usambazaji wa miche bora milioni 20 ya kahawa katika wilaya 52 na kufufua mashamba 150 yenye jumla ya hekta 400.

Mavunde alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi.

Mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali kufufua zao la kahawa nchini.

Mavunde alisema serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kufufua zao la kahawa hususan katika maeneo yenye mibuni iliyozeeka, mashamba yaliyotelekezwa na kuanzisha kilimo cha kahawa katika maeneo mapya.

Alibainisha kuwa mikakati hiyo inajumuisha uzalishaji na usambazaji wa miche bora ya kahawa na kuimarisha maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa ili kudhibiti magonjwa na kuongeza kasi ya uzalishaji wa miche bora.

Aidha, mikakati mingine ni kuboresha mifumo ya masoko ya kahawa ili kumlinda mkulima, kuwezesha matumizi ya teknolojia za umwagiliaji kwenye mashamba ya kahawa na kuimarisha utafiti na maendeleo kupitia Kituo cha Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI).

Alisema katika msimu wa mwaka 2022/23 jumla ya miche 8,784,146 ilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima na kati ya kiasi hicho, miche 5,458,123 ni aina ya arabika na 3,326,023 ni aina ya robusta.

# 'Wenye ulemavu washirikishwe ngazi za mitaa, kata'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

OFISA Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Pwani, Grace Tete, amesema kundi la watu wenye ulemavu linatakiwa kushirikishwa kwenye kamati zinazoundwa kuanzia ngazi ya mitaa na kata.

Tete amesema viongozi wanatakiwa kutambua kwamba kwa kushirikisha kundi hilo itakuwa rahisi kujua vikwazo wanavyokumbana navyo na kuvitafutia ufumbuzi.

Alibainisha hayo alipokuwa akifungua semina kwa watu wenye ulemavu, wenyeviti wa mitaa na watendaji kutoka kata sita za Wilaya ya Kibaha, iliyofanyika kwa ufadhili wa Shirika la The Foundation for Civil Society.

Alisema kuwashirikisha watu wenye ulemavu kwenye kamati na mambo mbalimbali, inasaidia wawakilishi wao kuwasilisha kero zao ziweze kufikia mamlaka za juu na kushughulikiwa.

Aidha, Tete amewaelekeza viongozi hao kuzingatia kuwa na takwimu sahihi za watu wenye ulemavu ili inapoibuliwa miradi waweze kunufaika kama ilivyo kwa wengine ambao hawana ulemavu.

"Makundi yote yashirikishwe kufikisha hoja zao tuhakikishe wanapata huduma zinazotolewa na wajumuishwe kwenye kamati zinazoundwa, 2024 tusiwaache kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa washirikishe kwa kila hatua kujenga usawa," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa CHAVITA, Mkoa wa Pwani, Festo Christian, alisema wenye ulemavu wakishirikishwa vizuri itasaidia kuwaondolea vikwazo.

Mjumbe wa chama hicho, Tatu Kondo, alisema semina hiyo ni mwendelezo wa mradi ulioanza mwaka jana na haukuwa na matokeo chanya isipokuwa kata moja ya Kongowe.

Kwa mujibu wa Kondo, wafadhili wameamua kuendeleza ufadhili wao ili kuleta mabadiliko kuanzia ngazi ya mitaa kwa kuwapo kwa ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu kwenye kamati mbalimbali zinazoundwa.

Mtendaji wa Kata ya Visiga, Aloycia Nyelo, alisema kwa kuzingatia mafunzo waliyopatiwa, anatarajia kuyafanyia kazi kwa kushirikisha kundi la watu wenye ulemavu katika shughuli mbalimbali.

Nyelo aliahidi katika uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa kushirikisha kundi hilo kwa kila hatua ili nao waweze kujumuika na wengine kushiriki kuomba kuchaguliwa kuongoza kwenye maeneo yao.



# Mgogoro wasababisha mgodi wa dhahabu kufungwa

**Na Mwandishi Wetu,** HANDENI

MGODI wa dhahabu ulioko Kijiji cha Kwandege, Kata ya Lang'ata, Wilaya ya Handeni mkoani Tanga unaomilikiwa na Godfrey Bitesigirwe, umefungwa kutokana na mgogoro baina ya mmiliki na wachimbaji wadogo.

Mgogoro huo unadaiwa kuchochewa na madalali ambao wametanguliza mbele maslahi yao na hivyo kuathiri uwekezaji na mapato ya serikali.

Ofisa Mfawidhi wa Madini, Mkoa wa Tanga, Zabibu Napacho, alisitisha shughuli za uchimbaji katika mgodi huo, Juni 6 mwaka huu.

Mgodi huo ulipewa leseni ya uchimbaji mdogo na uchenjuaji madini, ukiwa umesajiliwa kwa PML 0330-0337 TNG-Kwandege.

Alisema agizo hilo linatokana na kikao cha pamoja kati ya Mkuu wa Wilaya hiyo na kamati yake ya ulinzi na usalama, viongozi wa chama, serikali na mmiliki wa mgodi huo, kilichofanyika katika Shule ya Msingi Kilimazinga.

Aidha, sehemu ya barua hiyo ya Ofisa Madini inaeleza: "Mkuu wa Wilaya ya Handeni ameniagiza kusitisha shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa madini kwenye leseni zako PML 0330-0337 TNG zilizopo eneo la Kwandege, Kijiji cha Kilimamzinga ili kupisha kamati ya uchunguzi."

Hata hivyo, Bitesigirwe, kupitia barua yake kwenda kwa Mkuu wa Wilaya hiyo na mamlaka nyingine, ameeleza kutoridhishwa na agizo hilo na kutoa sababu nane za kupinga agizo hilo.

Moja ya pingamizi lake ni kupinga kuzuiwa kwake kuendesha shughuli za uchimbaji kwa kuwa agizo linatoa mwanya kwa uchimbaji usio rasmi kuendelea katika mgodi wake.

Kutokana na zuio hilo, mwekezaji huyo amemwomba Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, kutembelea mgodi huo ili kujionea sintofahamu ambayo imekuwa ikijitokeza baina yake na wachimbaji wadogo na kulipatia sakata hilo ufumbuzi ili aweze kuendelea na uzalishaji.

Kwa mujibu wa Bitesigirwe, alinunua mashine kubwa za kisasa za uchimbaji na uchenjuaji zenye gharama kubwa baada ya kuchukua mkopo Benki ya NBC, ambapo hutakiwa kurejesha kila mwezi, lakini kutokana na kusimamishwa kwa mgodi huo ameshindwa kufanya marejesho.

Alisema hana mgogoro wowote na wachimbaji wadogo wa dhahabu katika Kijiji cha Kwandege, bali kuna madalali wa dhahabu wanaosafiri kwenye migodi mbalimbali ya dhahabu nchini ambao ndio wanaochochea mgogoro huo.

Mwekezaji huyo mzawa alisema yeye anamiliki leseni nane katika eneo la Kijiji cha Kwandege alizopewa mwaka 2019 kwa kufuata taratibu zote za Tume ya Madini na alianza uchimbaji mwaka 2020.

Alisema katika muda wote hakuwahi kuwa na ugomvi na kijiji, wachimbaji wengine wala viongozi wa chama na serikali ngazi ya wilaya hatua ambayo anashindwa kujua ni sababu zipi zimesababisha yeye kusitishiwa shughuli za uchimbaji kwani sababu zilizoelezwa yeye anaziona hazina mashiko.

Akizungumzia tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Albert Msando, alikiri kumwagiza Ofisa Madini, kusitisha shughuli za uchimbaji dhahabu katika leseni hiyo baada ya wahusika kupewa muda mwingi kukaa chini kutafuta suluhisho na kushindikana.



Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Charles Shirima (kulia), akizungumza na Mkurugenzi wa Agruzania Inter, Sarfaraaz Rashid, wakati wa semina ya kujengea uwezo wajasiriamali kuhusu masoko ya mitaji kwa maendeleo ya uchumi, jijini Arusha jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanahabari wanawake watakiwa kuchangamkia fursa za uongozi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Jaji Imani Aboud, ameshauri waandishi wa habari wanawake waliopata mafunzo ya uongozi watumike kama chachu ya kupata uongozi mchanganyiko na wanaume.

Akizungumzajana jijjni Arusha wakati akifunga mafunzo ya siku tatu ya uongozi wa vyombo vya habari kwa waandishi wanawake waandamizi, Jaji Aboud, alisema hakuna anayepinga kuwa sekta ya habari kwa kipindi kirefu imekuwa na wanaume zaidi na utafiti uliofanywa umethibitisha kuwa wanaume wameendelea kuhodhi madaraka katika vyombo vya habari. "Pia maudhui ya vyombo hivyo bado hayajazingatia vya kutosha sauti za wasio na sauti, ikiwa ni pamoja na wanawake na makundi mengine ya pembezoni,"alisema

Jaji Aboud alisema utafiti wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) wa mwaka 2019 ulioitwa 'Breaking the Glass Celling' umethibitisha kuwa bado kuna upungufu hususanI katika nafasi za uongozi na pia maidhui yanazingatia usawa wa kijinsia katika vyombo vya habari.

Aidha, alisema mafunzo hayo yatakuwa ni dira ya kupata viongozi mahiri wanawake katika vyombo vya habari ambao watachangia kuleta mabadiliko katika sekta ya habari na hasa wanapopewa uongozi huwa mahiri na wenye weledi katika kusimamia haki zao.

"Hivyo natoa wito maalumu kwenu wahitimu kufanya kazi kwa bidii, ubunifu, weledi na kujiamini, kwa kufanya hivyo mtaweza kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi na ubora wa hali ya juu, kwani ni dhahiri wanawake wanaweza,"alisema.

Kwa mujibu wa Jaji Aboud, historia inaonyesha wanawake wameachwa nyuma katika suala la uongozi kwa kipindi kirefu na hivyo juhudi mbalimbali zimechukuliwa kikanda na kimataifa ili kuinua hali za wanawake kiujumla na hususani katika uongozi.

"Jitihada hizo ni pamoja na kuridhia masuala ya haki za wanawake na uongozi katika sera mbalimbali za kitaifa na mikataba ya kikanda na kimataifa,"alisema.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga alisema mafunzo hayo yanalengo la kuwajengea uwezo waandishi wa habari wanawake kwenye nyanja mbalimbali za uongozi, pamoja na maeneo mengine kama uandishi wa habari za uchunguzi.

Kajubi alisema MCT limefanikiwa madawati ya jinsia kwenye vyombo vya habari ili kuweka usawa wa kijinsia kwenye vyombo vya habari na kusisitiza uandishi wa jinsia zote kwa usawa.

# RC ahimiza utunzaji mazingira katika mazao ya misitu

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WANANCHI wanaoishi maeneo yenye mradi wa kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao ya misitu wametakiwa kulinda na kutunza mazingira ikiwa ni pamoja na vitendeakazi vya mradi huo vilivyoachwa baada ya muda wa mradi kumalizika.

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa alitoa wito huo jana kwenye kikao cha makabidhiano ya shuhuli zilizokuwa zinatekelezwa na programu ya kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao ya misitu kwa Wilaya ya Handeni na Kilindi.

Alisema mradi huo uliotekelezwa katika kipindi cha miaka minne umeleta ufanisi mkubwa kwa wilaya husika hivyo inawapasa wananchi walioko maeneo hayo kutunza vifaa vilitumika kutekelezea ili viweze kuendelea kufanyia kazi nyingine zitakazotokea.

"Wakurugenzi wote na wataalamu wa misitu ni vizuri mkaenda kuvisimamia vile vitendeakazi ili viendelee kuwepo, haitakuwa sawa mwisho wa siku mnarudi kwa walioacha mradi mnatoa changamoto zenu, vile vifaa visije vikageuka vya kuharibu misitu badala ya kutekelezea mradi" alisema.

Aliongeza: "Maofisa maliasili, kupitia elimu mliyoipata saa muende mkawajengee uwezo wananchi wenu ili wapate hizi taaluma wabaki nazo kuliko kuwaacha bila kupata tija kwa mradi huu, dunia sasa inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi, katoeni elimu wananchi waache kukata miti ovyo, badala yake wayatunze mazingira" alisisitiza.

Aidha Mgandilwa alipongeza Ubalozi wa Finland kwa kuleta mradi nchini kwani umetekelezwa ipasavyo na kuleta maendeleo kwa vijana wengi ambao wamejiajiri kupitia mradi huo.

"Niupongeze sana Ubalozi wa Finland kwa kutuletea mradi huu nchini kwetu, umetekelezwa kwa tija na umetuletea faida, niombe kama kutakuwa na miradi mingine mtuletee Tanga kwa maana zile wilaya zenye maeneo ambayo yanafaa kufanya mradi nazo zipate" alisema.

Naye Mratibu wa programu ya kuongeza thamani mazao ya misitu kitaifa, James Nshale, aliwataka vijana mkoani Tanga kujiunga kwenye vikundi na kujikita kwenye shuhuli za kujiajiri ili kunufaika na fursa zinazotolewa na serikali kwa kupatiwa mikopo ya halmashauri.

Nshale, alisema mradi huo umefanikiwa kwa kiasi kikubwa ndani ya miaka minne kwani maendeleo yameonekana na sasa vijana na wanawake katika wilaya husika wanaendelea na shuhuli za kujiajiri.

Alisema: "Vijana wa Wilaya ya Handeni na Kilindi ambao wamepata bahati ya kufikiwa na mradi huu, wamefanikiwa kujiunga kwenye vikundi na wamepatiwa mikopo ya halmashauri zao hivyo nitoe wito kwa vijana waweze kujifunza na kujiunga kwenye vikundi nao wapatiwe mikopo".





# RC aagiza uchunguzi madai mkurugenzi kumiliki kampuni

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla amemuagiza mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Idara ya Mipango pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuhakikisha wanachunguza na kufanyia marekebisho umiliki wa kampuni ya Misungwi Company Ltd inayomilikiwa na halmashauri baada ya Mkurugenzi kubainika kuwa mbia binafsi wa kampuni hiyo.

Kampuni hiyo yenye usajili Na.140457876 Novemba 21, 2019 ikiwa na mali za zaidi ya Sh. bilioni,35.54 na fedha taslimu zaidi ya Sh.bilioni 24.54 na mashine zenye thamani Sh.bilioni 11 huku ikiwa na udhaifu kwenye muundo na usimamizi na kukosekana kwa gawio la moja kwa moja kwa halmashauri hiyo.

Agizo la Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla lilitolewa juzi na Katibu Tawala Mkoa, Balandya Elikana wakati wa mkutano maalum wa baraza la madiwani kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema kuwa haiwezekani kampuni ya serikali ikaanzishwa na kuendeshwa kwa kukiuka taratibu za umiliki wa kampuni ikiwa ni pamoja na Mkurugeni wa Halmashauri kuwa mbia binafsi katika kampuni ya serikali.

Kadhalika aliitaka halmashauri hiyo kufanyia marekebisho ya mapendekezo ya CAG ili kuhakikisha Kampuni ya Misungwi Company Ltd inamilikiwa na Halmashauri kwa asilimia 100 na kuondoa kasoro hizo zinazoiingizia hasara serikali.

Vilevile, alitoa siku 30 kwa TAKUKURU kufanya uchunguzi ili kubaini uendeshwaji wa kampuni hiyo na kubaini sababu za kasoro hizo zilizopo katika muundo wa umiliki ikiwa ni pamoja na kuja na taarifa itakayoeleza sababu za mkurugenzi huyo kuwa mbia binafsi kinyume cha sheria.

Aidha, aliitaka halmashauri hiyo kuwa na mwenendo wa kushughulikia hoja za CAG kwa haraka ili kujihakikishia wanaendelea kupata hati safi na kwamba hilo linawezekana endapo watafuata taratibu na kanuni za mapato na matumizi ya fedha za umma.

Awali akiwasilisha taarifa kwa niaba ya mkurugenzi, Mweka Hazina wa Halmashauri hiyo, Ngugu Mazito alisema pamoja na kupata hati safi CAG alitoa hoja 16 ambazo zilitakiwa kujibiwa na kuwasilisha majibu kwa ajili ya uhakikiki.



Meneja wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Ziwa, Mhandisi Francis Mihayo akitoa mafunzo kuhusu majukumu ya mamlaka hiyo, sheria za mawasiliano ya kielektroniki na Posta na sheria za habari kwa waandishi wa habari wa Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# TASAF yatenga bil.1.9/- kuwafikia walengwa

**Na Neema Emmanuel,** MISUNGWI

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umetenga Sh.bilioni 1.9 zitakazowafikia walengwa 10,000 kutoka kaya maskini wilayani Misungwi mkoani Mwanza.

Fedha hizo zitawafikia kupitia ajira watakazozipata katika miradi 108 inayotekelezwa ndani ya wilaya hiyo ikilenga kuleta maendeleo na kukuza uchumi.

Hayo yamebainishwa juzi na Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Gloria Emmanuel, baada ya ukaguzi wa mradi wa bwawa la maji (rambo) wa Sh.milioni 18.8 uliojengwa na walengwa 122 kutoka Kijiji cha Mwakalima Kata ya Kanyelele.

Alisema katika miradi 108 inayotekelezwa wilayani humo ni pamoja na ufunguzi wa barabara na mabwawa ya maji katika vijiji 108 ambako miradi nane ni ya mabwawa ya kunyweshea mifugo na kilimo cha umwagiliaji.

Alisema miradi 100 ikiwa ni ya ujenzi wa barabara za jamii ambako walengwa wananufaika kwa kupata ajira za muda.

Gloria alisema wanufaika katika miradi hiyo wanalipwa Sh. 3,000 kwa siku na kufikia Juni 30, mwaka huu inatarajiwa kukamilika kwa asilimia 100.

Alisema mradi huo utawasaidia wananchi kuondokana na adha ya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, ujenzi, kilimo cha mboga, mahindi na mpunga pamoja na kunywesha mifugo.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mwakalima, Alogius Dokson alieleza kuwa wananchi wake wameondokana na adha ya kupotelewa na mifugo huku mazao yakiongezeka baada ya kukamilika kwa ujenzi wa bwawa hilo ambalo limeweza kuzinufaika kaya zaidi ya 486 zilizopo katika eneo hilo.

"Kijiji chetu kina ng'ombe 2,281, kondoo 331 na mbuzi 820 mifugo hiyo inatumia rambo hili. Pia kuna kilimo cha umwagiliaji nacho kinafanyika hapa, kwa sasa tunauwezo wa kulima mwaka mzima," alisema.

Mkazi wa Kijiji cha Mwakalima, Marco Luchemba alisema kupitia mradi huo wameweza kunufaika na ajira za muda mfupi kwa kujenga nyumba na kuondokana na upungufu wa maji ambapo awali hali ilikuwa mbaya.

# Wanaotaka kuanzisha vituo vya redio waitwa TCRA

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MENEJA wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Ziwa, Francis Mihayo, amawataka watu wenye uhitaji wa kuanzisha vituo vya redio kufika katika ofisi za TCRA kwa ajili ya kupewa miongozo na taratibu ili kuendana na matakwa ya kisheria.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa mafunzo ya waandishi wa habari wa Mkoa wa Shinyanga yaliyoratibiwa na TCRA yaliyokuwa na lengo la kufahamu majukumu ya mamlaka hiyo, sheria na kanuni zinazosimamia sekta ya mawasiliano ya kielekitronik na posta na sheria za habari.

Hivyo, aliwataka kuacha tabia za kutumia vishoka katika kuanzisha redio hizo na kuwahimiza waandishi wa habari kufuata sheria ya vibali vya mawasiliano yao pamoja na wale ambao wanaanzisha vyombo vya habari vya mitandaoni kusajili ili wasije wakaingia kwenye mkono wa sheria.


Naye, Mwenyekiti wa Mwanza Press Club, Edwin Soko alisema katika kipindi hiki cha sakata la bandari waandishi wa habari wanapaswa kuwa makini na uchapishaji wa maudhui yao ili kuepuka kutoa habari zisizo za uhakika.

Aidha, alisema waandishi wa habari wakiishi katika miiko yao na kufuata sheria na maadili ya kazi yao hakuna ambaye atajikuta ameingia kwenye mkono wa sheria sababu watakuwa wakifanya kazi zao kwa ufanisi na weledi mkubwa.



Ukurasa 12

Bosi Bodi Pamba, mwanaushirika wafafanua kwa kituo uzalishaji, bei pamba zilivyodondoka




Ukurasa 13

Tukae na Museveni usijege ukawa nyama


# BUFE

IJUMAA JUNI 23, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 14

**Zijue hatua mafanikio kiuchumi, iwe kwenye ajira hadi biashara**

UCHUMI

# Serikali Awamu ya Sita ikisonga na safari uchumi kwa mitaji PPP

• Dira ya bajeti; wateta na Benki Dunia...

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kila kipindi cha Bunge la Bajeti si jambo la ajabu kuwapo mijadala rasmi au isiyo rasmi, au yote kwa pamoja, kulingana na kitakachotokea kwenye hoja za maslahi ya jamii. Pia, matukio hayo huwa sio adimu.

Msingi huo unapovaliwa darubini, hata kwa uangalizi wa kawaida unavuka awamu mbalimbali za uongozi wa nchi, ikiwamo serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Ni hali inayotokana na siasa, pia uchumi, kwamba zimeshikamana na zinatumia kanuni ya pamoja, ikiwamo uchumi inaposimamia mlengo wa kulia, maana yake inatoa fursa kwa soko kutawala, serikali ikirejea nyuma kubaki msimamizi na mratibu, pia mnufaika wa kodi za sokoni.

Pia, kinyume chake kwa mfumo wa mlengo wa kushoto, serikali inakuwa mstari wa mbele kuzalisha, pia ikiwahudumia watu inaowatoza kodi kubwa, ili kupata uwezo sahihi wa kutimiza majukumu yake.

Ufafanuzi wake unapatikana kwa msisitizo aliopenda mwanazuoni wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam raia wa Sudan Kusini, Dk. Alfred Lokuji anayetamka "mlengo wa kushoto maana yake, serikali inadumu kuwa sehemu ya umma, haikubali kubaki nyuma ikawaacha watu wake (au mali zake) waumizwe na nguvu ya soko."

Hata hivyo, kiuhalisia hakuna serikali duniani inayoegemea upande mmoja kwa asilimia zote. Sifa ya uchumi mlengo wa kulia, ni ushindani wa soko unaleta tija katika uzalishaji na mauzo sokoni.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, alipoongoza kikao jijini Dodoma, kati ya serikali na ujumbe wa Benki ya Dunia (WB), kujadili namna bora ya utekelezaji Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), pia uboreshaji mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini. **PICHA: MTANDAO**

Vilevile, kwa mfumo wa kushoto unazaa kinga kutetea na kulinda wanaolemewa na nguvu ya soko, ambao wanaouhimili ndio huangukia ushindi na wanaoshindwa, pamoja na mali zao wanabaki katika hali mbaya. Hapo ndipo serikali huiingilia kati kuchukua hatua za nusura.

Hiyo ni nadharia inayowaangukia watu na mali zao. Itakumbukwa nchini, mfano hao ni baada ya serikali kuchuukua hatua ya kubinafsisdha taasisi za umma, Shirika la Reli Tanzania, lilibinafsishwa kwa hatua ya kukodishwa.

Muda mfupi baada ya kugundulika mwekezaji aliyebinafsishiwa shirika hilo kwa njia ukodishaji miaka 20, tija ikawa duni, serikali ikaingilia kati ikauvunja mkataba na TRC, ambayo ilishabadilishwa jina, kuwa Kampuni ya Reli Tanzania (TRL), ikarejeshwa kubaki shirika la umma kawa awali hadi sasa.

Juhudi za maboresho yake, ndiyo yanaendelea sasa ikitolea ufafanuzi kila mara na Rais Dk. Samia, katika moja ya miradi mikubwa katika serikali ya awamu ya sita, ikiurithi kutoka awamu zilizopita, TRC kupitishia treni zake katika reli ya kisasa, ikiwa katika hatua za ukamilshaji na baadhi ya mabehewa yameshaletwa nchini.

**AWAMU YA SITA NA PPP**

Kiuchumi, sekta binafsi mara zote ni wakala mkuu wa nguvu ya soko, kwani ndio wanaotimiza uzalishaji na mauzo sokoni.

Historia nchini, katika mabadiliko ya kipindi cha awamu ya nne ya uongozi wa nchi, chini ya Rais Jakaya Kikwete, kukabuniwa sera na sheria, inayojenga rasmi ubia wa mipango na uchumi kati ya serikali na sekta binafsi, maarufu PPP (Public na Private Partnership).

Kuundwa PPP, mzizi wake unaanzia mageuzi ya kisera nchini mwaka 1985, pale sera za nchi zikabadilika kiuchumi kutoka mfumo hodhi, hadi ulingo wa soko na kwa kiasi kikubwa ilikuwa kipindi cha mageuzi.

Baadaye mwaka 1995, kwenye serikali awamu ya tatu, Rais Benjamin Mkapa, akafahamisha msimamo wa serikali ni kujiengua kwa kiasi kikubwa katika mfumo wa uzalishaji na kuhudumia bidhaa sokoni, yenyewe ikibaki mratibu uchumi.

Ni kipindi kukashuhudiwa kuundwa wizara kama za utawala bora, pia kuendelezwa wakala nyingi za kusimamia majukumu ya kiserikali.

Kupitia mtazamo huo wa kiusimamizi, ndio kwa kiasi kikubwa katika serikali ya awamu ya sita, inatumia sababu PPP, katika kufakinisha majukumu yake kibiashara, kiuchumi na huduma za umma.

Hadi sasa katika serikali ya awamu ya sita, kuna mjadala unaoendelea kuhusu mkataba wa awali wa ubinafsishaji bandari nchini, ambao katika namna pana umejikita katika maudhi ya mkataba.

Nako ikirejewa hadi kufikiwa mkataba huo, ni ndani ya kutafuta tija kiuchumi kupitia sera ya PPP, ambayo sasa imeshika kasi duniani.

**KINACHOENDELEA SASA**

Kiutawala, vilevile kuna wakati serikali inaingilia kati mwenendo wa mlengo wa kulia wa soko wa PPP kwa kutetea maslahi ya umma kwa watumiaji na ndicho kinachoshuhudiwa kwenye utawala wa serikali ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kupitia anachowasilisha Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba bungeni.

Mfano hai, ni pale serikali ya awamu ya sita wiki hii ilipoondoa baadhi ya tozo kwenye simu kumlinda mtumiaji wa kawaida, muswada wake uko njiani kutua bungeni, baada ya kuwapo katika matumzi katika kipindi kifupi.

INAENDELEA UK.14

BIASHARA

# Bosi Bodi Pamba, mwana-ushirika wafafanua kwa kituo uzalishaji, bei pamba zilivyodondoka

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

• Mwaka huu; kutoka Sh.1560 za mwaka hadi Sh. 1,060...

KITAIFA, pia nchi nyingi za Kiafrika, sekta inayoajiri sehemu kubwa zaidi ya wananchi ni katika uzalishaji wa kilimo, ndio ikiwa mtaji muhimu wa maendeleo ya Watanzania, wakiwamo wanaoishi mijini wakitegemea mazao ya chakula na biashara kutoka shambani.

Mmoja wa wakala wenye mchango kuinua kilimo kuanzia uzalishaji hadi masoko, ni vyama vya ushirika nchini. Mkoani hapa, kuna mdau Chama Cha Ushirika Nyanza Co-operative Union 1984 Ltd (NCU), inayojikita katika uzalisha pamba, huku kuna mamlaka ya juu msimamizi, Bodi ya Pamba Tanzania.

Kimsingi, juhudi za uzalishaji katika eneo mojawapo, imekuwa ikiathiriwa na kushuka bei ya mazao sokoni na hapo inaguswa zao la pamba, ikiwamo wilayani Kwimba, anakopatikana mwanaushirika, Julius Mayala, akielezea changamoto inayowakabili wakulima ni kuwapo bei elekezi inayowashushia kipato, akirejea na msimu wa mavuno uliopo sasa.

Mayala anaeleza kwamba, kuyumba kwa bei ya kuuzia zao la pamba katika msimu uliopo, mwaka 2023, bei ikishuka kutoka Sh. 1560 kwa kilo hadi Sh. 1,060, inatokana na anachokitaja kuanzishwa kwa soko huria mwaka 1992, wakulima wakaanza kuuzia kampuni binafsi za kununua zao hilo.

Anasema kabla ya hapo, kulikuwapo vyama vya wakulima vilivyonunua pamba, akitoa mfano mkoani Mwanza, walikuwa na Chama Kikuu Cha Ushirika Nyanza Co-operative Union 1984 Ltd (NCU). Kwa mujibu wa Mayala, mkoani Mara kulikuwapo Mara Co-operative Union (MCU), vilevile Shinyanga ikawa na SHIRECU iliyohudumia hadi Chato, ambako sasa ni mkoa wa Geita.

Mayala anasimulia kwamba, baada ya kuingia soko huria pamba ikawa ya kunyang'anyana sokoni baina ya vyama hivyo vya ushirika na kampuni binafsi, ndiko kulikoanza kutokea ukiukwaji wa udhibiti na upatikanaji wa pamba bora, yenye kiwango kinachotakiwa.



Mkulima akihudumia shamba lake la pamba. **PICHA: MTANDAO**

> **Kuna yanayotajwa na Bodi ya Pamba, kwamba hazikuwapo mvua za kutosha na kuathiri mazao, wakulima kutokuwa na elimu ya kutosha kulima mazao bora.**

Mayala anataja hali iliyofikisha kukosekana pamba safi au usafi, hata ikashusha thamani kwenye soko la dunia, usimamizi wake kwa wakulima ukadorora, pamba ikizalishwa kiholela pasipo kuzingatia kanuni na usafi wake.

Anataja namna kampuni zilivyowalipa wakulima bei kubwa na 'keshi' bila mkopo, ikiua ushindani wa kununua zao hilo dhidi ya vyama vya ushirika.

Mayala anataja hali hiyo ikawasukuma wakulima kupata nafasi ya kuweka mchanga, maji, mawe, mafuta ya kenge na vitu vingine wenye pamba wakati wa kuuza, lengo ni kuongeza uzito kwa kila kilo.

Pia, mwanaushirikia huyo anakumbusha enzi zilizopita, kilicho chao kilisimamiwa na mabwana shamba, ili wazingatie kanuni za kilimo bora, lakini baada ya kuwapo soko huria, vyote hivyo vilitoweka,hata wataalam hao hawakuweza kuwatembelea tena kukagua mashamba yao.

Anataja kuwa ni hali iliyowasababisha wakulima kuanza kulima kilimo cha kuchanganya mazao mengine kwenye pamba, nayo ikachangia uzalishaji wake kushuka na ukukikosa tija, kutokana na kanuni za kilimo kutozingatiwa tena.

### BODI YA PAMBA

Bodi ya Pamba Tanzania(TCB), katika hilo inafafanua zaidi kuhusu kushuka bei elekezi ya zao la pamba katika msimu uliopo wa kilimo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo,Renatus Luneja, akitaja ni jambo la kawaida, kushuka na kupanda kwa bei ya mazao ya biashara, akitoa mifano ya pamba, kahawa na tumbaku.

Luneja anafafanua kwamba, kushuka kwa bei elekezi ya kuuzia pamba katika msimu uliopo, kufikia shilingi 1,060, kutoka shilingi 1,560 za msimu uliopita 2022, kumesababishwa na mtikisiko wa vita vya Russia na Ukraine, pamba ikiathirika katika soko la dunia..

Mkuu huyo wa Bodi ya Pamba nchini, anafafanua kwenye msimu wa mwaka jana, bei ilipanda zaidi kutoka shilingi 1,560 kwa kilo, hadi kufikia shilingi 2,100 na baadaye ukiwa unaendelea, bei ikashuka tena kurudia hali ya awali.

Anaeleza, kupanda bei mwaka jana, kulisababishwa na kuwapo ugonjwa Uviko 19, bei ikienda juu katika soko la dunia, kwa sababu nchi nyingi zilishindwa kuzalisha zao hilo, kutokana na kuathiriwa na ugonjwa husika.

Luneja anasema nchi zinazoongoza kulima pamba barani Afrika ni: Mali, Burkinafaso, Ivory Coast na Tanzania, huku barani Asia inagusa nchi za India, China, Marekani na Brazil, wakati nchi zenye viwanda vikubwa vya pamba ni Singapore, Pakstan, India na Bangladesh.

Vilevile kuna nchi za Ufaransa na Ujerumani, nazo zikitajwa katika orodha ya kuwa vinara wa ununuzi wa zao hilo, kwa ajili ya kutengeneza nguvu maalum za kibiashara. Anaamini kwamba suluhu ya kilimo hicho ni pale mkulima anatakiwa kulima kilimo bora na chenye tija, ili kutoa elimu kupitia vyombo vya habari, mikutano mahsusi ya hadhara, vipeperushi na mashamba darasa, pia serikali kuhakikisha mkulima anapata pembejeo za kilimo,

Mfano uko katika mbegu,viuadudu,vinyunyizi na, zana zingine za kilimo, kama vile majembe ya palizi na majembe ya kupandia kwa wakulima wote, ikiwa ni pamoja na pembejeo zote, kutolewa kwa mkopo kwa wakulima, kwa ajili ya kilimo bora ili kuongeza zaidi uzalishaji wake.

Aidha, mkulima hulipa pembejeo kupitia kujengeka bei husika na hakatwi moja kwa moja,kupata elimu ya matumizi sahihi ya dawa za viuadudu na vinyunyizi kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea (TPHPA)

Mamlaka hiyo huchukua sampuli hizo na kuziingiza maabara za vipimo, ili kuthibitisha dawa hizo, zina ubora, pamoja na bodi hiyo kuzithibitisha ubora wa matumizi zinapofika kisha kuzisambaza kwa wakulima.

### CHANGAMOTO KUU

Malalamiko ya wakulima kuhusu dawa, viuadudu na vinyunyizi kushindwa kuua wadudu, kunatokana na kutofuatwa kanuni za matumizi sahihi, ukiwamo uchakachuaji au mtumiaji kupunguza kipimo.

Hivyo, kushindwa kuua wadudu,kutotumia wataalamu wa kilimo au kuzidisha na kusababisha kuathiri mimea.

Mabadiliko ya tabia nchi nayo yamesababisha zao hilo kulimwa popote, tofauti na zamani palikuwapo kanuni kulingana na hali ya hewa ya eneo husika, ikiwamo mbegu za pamba zinazozalishwa katika mikoa ya Katavi na Tabora, hasa wilayani Igunga.

Baada ya hapo, inatajwa mbegu hizo zinsambazwa kwa wakulima wa mikoa mingine, ambazo zimefanyiwa utafiti wa kutosha kuhusu wake katika kilimo.

Matarajio ya Bodi ya Pamba msimu uliopo, yanatajwa ni kwa wakulima walime jumla ya ekari milioni 1.8 hadi unapofunguliwa msimu mwezi Mei, kilimo kikitosheleza ekari milioni moja pekee,chini ya lengo lao la uzalishaji.

Hali kadhalika suala la malengo kutofikiwa kutokana na sababu mbalimbali kama mabadiliko ya tabianchi, hali ya hewa, huku wakulima wengine wanajitoa wakati washalichukua mbegu, kuchanganywa mbegu za pamba na mazao mengine, yakiwamo ya biashara na chakula wakati wa kulima.

Aidha, kuna yanayotajwa na Bodi ya Pamba, kwamba hazikuwapo mvua za kutosha na kuathiri mazao, wakulima kutokuwa na elimu ya kutosha kulima mazao bora.

Hadi sasa inatajwa ni kati ya asilimia 60 hadi 70 ya wakulima wanazingatia kanuni za kilimo bora nchini, pia kuwapo Sheria ya Pamba ya Mwaka 2001, inayomzuia mkulima kuchanganya zao hilo na mengine, akibainisha adhabu yake ni kifungo cha miezi mitatu jela au faini shilingi 200,000.

### MIKAKATI YA TCB

Kaimu Mkurugenzi, Luneja, anasema mikakati waliyo nayo ni kuwapa wakulima elimu na kuwataka kubadilisha teknolojia za kilimo na nafasi za upandaji mbegu za pamba, ili kuongeza tija ya uzalishaji kwa mkulima.

Lingine analolitaja ni suala la kuboreshwa usambazaji pembejeo za kilimo, ikiwamo dawa na mbegu za kuongeza shughuli za utafiti kwenye pande zenye uzalishaji mkubwa, ili kuangalia ukame, magonjwa na wadudu husika.

Vilevile katika upandaji mbegu kwenye mashimo husika, Luneja anaelimisha ni umbali wa sentimita 30 kati ya mstari shimo moja na lingine, tofauti na zamani ilikuwa sentimeta 40.

Pia, umbali kati ya mstari mmoja na mwingine kwa sasa unatakiwa na bodi kuwa sentimeta 60, huku mabadiliko yaliyoko sasa ni sentimita 90.

## Serikali Awamu ya Sita ikisonga na safari uchumi kwa mitaji PPP

**INATOKA UK.11**

Mnamo Machi mwaka huu, wakati akikutana na ujumbe wa Benki ya Dunia, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, akasema ni majadiliano ynayotokana na utekelezaji wa msisitizo na maelekezo ya Rais Dk. Samia, kwamba ni wakati wa sekta binafsi kushirikiana na serikali, kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Ilikuwa kwenye kikao kati ya serikali na ujumbe wa Benki ya Dunia, kujadili namna bora ya utekelezaji PPP na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji, katika ufanyaji biashara nchini.

Naibu Katibu Mkuu anasema, serikali inafanya majadiliano ya kimkakati na Benki ya Dunia, kupata namna bora ya kuiwezesha sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji miradi ya maendeleo, kupitia PPP iliyoko kisera na kisheria sasa.

Ni kikao ambacho, pia kilimhusisha Mkurugenzi Mkazi wa Benki hiyo, Nathan Belete, katika mjadala ambao uligusa namna bora ya utekelezaji sheria ya PPP.

Kwa mujibu wa Mafuru, Rais Dk. Samia, msisitizo wake unagusa inapotokea penye uwezo wa sekta binafsi kutekeleza mradi kwa fedha zake, serikali inahamisha mtaji wake kuhudumia mengine.

"Wenzetu wa Benki ya Dunia wamekuwa mstari wa mbele katika kutoa fedha sio tu katika miradi ya kijamii, lakini sasa wanajielekeza zaidi kutoa fedha na misaada ya kitaalamm kuhakikisha kwamba eneo hili la PPP, sambamba na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara nchini yanafanikiwa," anfafanua Mafuru.

Pia, anadokeza hatua ya serikali kuanza majadiliano ya awamu ya pili na Benki ya Dunia, kuhusu msaada unaojielekeza kwenye sekta za miundombinu na sekta zitakazoboresha mazingira ya kufanya biashara nchini.

Pia akataja, sheria ya PPP inafanyiwa marekebisho, ili iweze kuwa shindani, kuwezesha kuvutia mitaji ya sekta binafsi, hali inayoaminika itamirisha ushirikiano katika kutekeleza miradi husika.

Naibu Katibu Mkuu, anasema ni hatua itakayopunguzia serikali mzigo wa kibajeti, ili fedha zilizopangwa kwenye miradi, inaweza kuachiwa sekta binafsi zielekezwe kwenye huduma za kijamii, ambazo haziwezi kuvutia sekta binafsi.

### BENKI YA DUNIA

Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia, Nathan Belete, anasema benki hiyo imeamua kujadiliana na Tanzania namna bora ya utekelezaji wa miradi kwa njia ya PPP, kwa kuwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Rais Dk. Samia.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Tukae na Museveni usijege ukawa nyama






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

KUNA mkazi wa Afrika Mashariki, anaitwa Asuman Basalirwa. Huyu ni Mbunge wa Bunge la Uganda jimbo la Bugiri, Manispaa ya Bugiri.

Basalirwa amefanya jambo kubwa sana nchini mwake, pia Afrika Mashariki na pengine tuseme Afrika, kwa kuwasilisha bungeni muswada wa kupinga mapenzi ya jinsia moja au ushoga.

Baada ya kuwasilisha muswada huo na kujadiliwa na wabunge, hata ukapitishwa na idadi kubwa kama si wote, hatimaye Rais YoweriMuseveni, akautia saini kuwa sheria.

Uamuzi huo wa Rais Museveni unapingwa wazi wazi na baadhi ya mataifa makubwa, yakiongozwa na Marekani, ambao mara moja taifa hilo likafuta viza za Spika wa Bunge hilo, Anita Among.

Hata baada ya Marekani kutangaza hatua hiyo, wabunge wa Uganda wakasema, ikitaka izuie pia viza za Museveni na wabunge wote, kwa sababu uamuzi wa kupambana na ushoga ni wa wote.

Kwa mujibu wa sheria hiyo mpya iliyoanza kutumika mwaka huu, mara tu baada ya kusainiwa na Rais Museveni, hivi sasa mtu atakayepatikana na hatia ya kuchochea mapenzi ya jinsia moja, atakabiliwa na adhabu ya kifo.

Atakayekutwa na hatia ya kujihusisha moja kwa moja na mapenzi hayo, atakabiliwa na adhabu ya kifungo cha miaka 20 jela, sawa na atakayebainika anatetea na kutangaza mapenzihayo.

Hali kadhalika, mtu atakayebainika na kuthibitishwa anatoa mafunzo ya mapenzi ya jinsia moja kwa watoto, kwa mujibu wa sheria hiyo mpya, naye atakula mvua ya miaka 20 jela.

Kifungo cha miaka 14 jela kitamhusu atakayepatikana na na hatia ya kujaribu kuchochea aina hiyo ya mapenzi, huku miaka 10 ikimkabili atakayekutwa na hatia ya kujaribu kufanya mapenzi hayo.

Mtu atakayepatikana na hatia ya kumiliki taasisi au majengo yanayotumika kufundishia mapenzi ya jinsia moja, miaka 10 jela itamhusu, huku mtoto atakayebainika kuhusika na vitendo hivyo, akisukumwa jela miaka mitatu.

Wamiliki wa vyombo vya habari nao hawakuachwa nyuma, kwani atakayebainika chombo chake kinachapisha au kutangaza habariz inazotetea au kuhamasisha mapenzi ya jinsia moja, atapigwa faini ya Sh. Bilioni moja na kusimamishiwa leseni yake kwa miaka 10.

Baadhi ya vigogo wa dunia waliojitokeza hadharani kupinga hatua ya Uganda ni pamoa na Rais Joe Biden wa Marekani, aliyesema hilo ni janga dhidi ya haki za binadamu akiungwa mkono na Mkuu wa Sera wa Umoja wa Ulaya (EU), Josep Borrell aliyesema ni ukiukwaji wa sheria za kimataifa za haki za binadamu.

Wote wakatishia kuwa hatua hiyo itasababisha Taifa hilo litengwe kimataifa na kunyimwa misaada, huku wabunge wa Uganda wakisema hata kama misaada haitaletwa, watajipanga na kupunguza au kuacha na kusailiwa na kidogo walicho nacho kiwasukume.

Hata hivyo, wakasema watashirikiana na mataifa rafiki yanayopinga mapenzi hayo duniani, ili kuziba pengo la Marekani na washirika wake, ambao ni wapenzi wa mapenzi hayo.

Hakika Museveni na watu wake wanapaswa kupongezwa kwa kiwango cha juukwa kutambua jinsi binadamu wanavyotofautiana na wanyama kivitendo, lakini pia kutambua kuwa kumbe kuna binadamu wanazidiwa akili na wanyama.

Kama wanyama hawawezi kufanya vitendo hivyo vinavyotetewa na wakubwa hao, iweje nchi zingine za Afrika kote zikae kimya bila ya kuunga mkono mwenzao aliyethubutu?

Hivi binadamu anashindwaje kulinda haki zake na badala yake azidiwe na wanyama wasioweza kujadili chochote? Hivi tutakubali kuuza utu na kuonekana binadamu kwa sababu tu ya misaada?

Mnyama dume hawezi kufanya mapenzi na dume mwenziwe, hali kadhalika jike na jike, achilia mbali ndege, wadudu na samaki, iweje sisi tulioumbwa na Mungu kuwatawala, tunazidiwa nao akili na kufanya tuyafanyayo?

Pengine haya tunayosikia leo, wanyama wamevamia kijiji na kuuawa tunakufanya uharibifu, ni kwamba wanyama wameshatambua binadamu hatuna akili tena ya ubinadamu na hivi sasa ni wakati wa kubadilishana na wanyama, wao waje majumbani nasi tuhamie porini.

Nafasi na wadhifa tuliopewa na Mungu, polepole tunauvua na kuvika wanyama ambao baadaye si ajabu, wakatuzidi kila kitu nao ikawa zamu yao kututawala kutokana na kuharibikiwa akili,tunakokuona sasa. Tuamke tupambane na ushoga bila kuona aibu. **Alamsiki!**

UCHUMI

# Zijue hatua mafanikio kiuchumi, iwe kwenye ajira hadi biashara

**Na Luther Mugosha**

MTU anapotaka kufanikiwa kuna kanuni za mafanikio zilizokusanywa, hata kumuwezesha kupata anachokitaka maishani, ikiwamo uhuru wa kiuchumi.

Ni kanuni zimewekwa kwenye vitendo na mamia ya watu kwa takribani kila nyanja ya maisha, ili kuleta matokeo chanya na imewezesha kuwapa watu fedha nyingi, hata kuzifanya ziwe za kufikirika kimaendeleo.

Zinapatikana kila mahali na watu wanaweza kuzifikia kirahisi, hata kuuwezesha umma kunufaika kwa pamoja kupitia usemi wa Kiswahili "kizuri kula na wenzio".

Kanuni hizo za mafanikio zimethibitishwa na wanasaikolojia mashuhuri, hata kutumiwa na wavumbuzi na matajiri duniani.

Mara zote kunatajwa 'mafaniko ya kweli ni kuweza kumaliza kufanya kazi fulani kwa ufanisi au kufanikiwa kupata matokeo tarajiwa.'

## NAFASI YA HUDUMA

Kiasi kikubwa cha huduma kinatajwa ni kanuni ya mafanikio. Ipo kaulimbiu ya biashara "hupata faida sana, yeye anayehudumia vizuri sana."

Hiyo ni moja ya kaulimbiu nzuri sana katika biashara na maarufu sana na huwa inafanyakazi tu, endapo mfanyabiashara husika ataelewa maana ya maneno "anayehudumia vizuri sana" huwa yana maanisha kiasi 'kikubwa cha huduma' na sio 'huduma kidogo' inayotazamiwa au huduma ya kawaida tu.

Wafanyabiashara wengi wanajitahidi kutoa huduma tarajiwa au za kawaida tu na kuna wakati kuna huduma pungufu ya kilichotarajiwa, hata kufanya zisilete matokeo chanya; makubwa au mafanikio.

Penye huduma za kawaida, au tarajiwa inamuwezesha mfanyabiashara kupeleka mkono kinywani pekee, lakini inakuwa ngumu kumfikisha penye mafanikio.

Mojawapo ya njia za uhakika za kupata mafanikio ni kutoa, kutumia kiasi kikubwa cha huduma, bila ya kufikiria kupata faida ya haraka.

Kadri wateja watakavyoona wanafaidika moja kwa moja na huduma itolewayo na biashara, ndivyo utakavyowavutia zaidi na wanakuona unawasaidia. Kwa hiyo, watajisikia kutoka mioyoni mwao kurudisha fadhila.

Ni fadhila kutoka kwa wateja, ndiyo inarudishwa kwa kutumia vipato vyao zaidi katika huduma yako na kuwaletea wateja wengine kutokana na sifa ya kutoa kiasi kikubwa cha huduma na hatimaye mafanikio yanaanza kutokea.

Swali linaweza kujitokeza, iko wapi nguvu ya ziada? Au kitu gani cha ziada ambacho wengine hawana? Hilo huulizwa hata katika usaili au mahojiano ya kazi. Hapo kinachotafutwa ni hiyo ziada yako, yaani kiasi kikubwa cha huduma.

Nguvu hiyo ya ziada inayomtofautisha mfanyabishara na wengine wengi. Nguvu ya ziada inamfanya mtu aonekane na ubora tofauti na wengine, hata inampatia mafanikio au chochote anachotaka.

Inafahamika kwamba, maswali mengi hujitokeza, kama 'itatolewaje ya ziada na nguvu ya kuhimili gharama hiyo?'

## PATA KAZI KWANZA

Uhalisia ni kazi zipo kila mahali, lakini zinaweza zikawa ndogo kwa mhitaji. Hivyo, mtu anachohitajiwa kuwa nacho ni unyeyekevu kazini, kama mwenye busara mmoja aliyewahi kutamka, kunukuliwa "watu ambao wanaonekana ni wakubwa sana hushindwa kufanya vitu vidogo. Pia, wataonekana ni wadogo sana, kushindwa kuhitajika kufanya vitu vikubwa".

Rais wa kampuni moja iliyoanza biashara yake mwaka 1973, hata kufika mwaka 1977, tayari mapato yake yalikuwa fedha za Marekani Dola bilioni 90 kwa mwaka, akifafanua:

"Miaka saba kabla sijaanza biashara yangu, nilifanya kazi kwenye kampuni iliyokuwa inamilikiwa na ndugu zangu wa mbali. Ingawaje nilikuwa sehemu ya wanafamilia, bado nilikuwa nalipwa ujira mdogo sana.

"Bado nilifanya kazi sana kama mimi ndiye mmiliki wa kampuni. Sikuwa ninasubiri wengine, kwa juhudi nilitafuta shughuli za kufanya katika kampuni hiyo.

"Kamwe, sikuwahi kuchelewa kazini, wala kupumzika, yaani kutoenda kazini hata siku moja, kwa sababu nilisukumwa na furaha ya kupenda mafanikio. Bado ninafanya kazi kwa juhudi hadi leo."

Kimsingi, kuna njia moja inayotegemewa sana kupata utajiri kihalali, nayo ni kutoa huduma muhimu. Hakuna mfumo wa kiuchumi duniani, ambao watu kwa halali wanaweza kupata utajiri mkubwa bila ya kulipa thamani inayofanana na utajiri huo, katika namna moja au nyingine





Wajasiriamali tofauti wakiwa kwenye nyendo zao kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Miaka saba kabla sijaanza biashara yangu, nilifanya kazi kwenye kampuni iliyokuwa inamilikiwa na ndugu zangu wa mbali. Ingawaje nilikuwa sehemu ya wanafamilia, bado nilikuwa nalipwa ujira mdogo sana.**

## FURSA KATIKA UTAJIRI

Tanzania ina uhuru na fursa zote zinazohitajika, kuboresha uchumi, ambao mtu yeyote makini anahitaji. Mtu akienda kuwinda wanyama kwa ajili ya kitoweo, huwa anachagua upande ambao kuna wanyama wengi.Tunapotafuta uhuru wa kiuchumi kanuni hiyo hiyo hutumika.

Tanzania hutumia fedha Sh trilioni 1.3 kuleta bidhaa za vyakula kutoka nje kila mwaka kwa mujibu wa taasisi ya IFAD (International Fund for Agriculture Development), ikisema programu ya kilimo ya ASDP iliyozinduliwa mwaka 2018, inatoa kila kitu kinachohitajika kuboresha kilimo nchini.

Katika mwaka wa fedha 2022-2023, kunatajwa serikali nchini imetenga Sh. bilioni 294 kwa ajili ya kilimo.

Unatajwa uhuru wa Tanzania umekuwa msaada kwa yeyote. Hakuna chochote cha kumzuia mtu au yeyote kujihusisha au kuwa sehemu ya rasilimali katika kufanya biashara

Msingi wake ni kwamba, Tanzania inamhakikishia kila mtu kufanya biashara kwa kutoa huduma muhimu na kupata mapato yanayowiana na thamani ya huduma yake! Kuna fursa zimejifunua kupiga hatua mbele,

Inatajwa, chaguo la leo ndio linahamia katika biashara inayoanzishwa kesho. Pia, thamani ya kinachofanyika leo, ndicho kinaakisi ubora wa thamani ya mwanzo wa shughuli kesho. Muhimu ni mtu kutafakari au achukue hatua kuboresha thamani inayolindwa isishuke

## KAZI YENYE HUDUMA

Hakuna uwekezaji unaozalisha faida kwa siku moja. Kila uwekezaji unachukua muda kuzalisha faida. Mtu hawezi kupanda mahindi shambani leo na akaenda kuvuna wiki inayofuata.

Vilevile, mafanikio sio hadhi, bali huduma na msingi wa mafanikio ni huduma.Ni hiari ama mtu kujituma au kuhudumia, asonge kukaribisha mafanikio.

Kila mtu aliyefanikiwa, huwa ana msukumo huo amejiwekea ndani yake, yaani shauku ya kuchangia kitu kutatua tatizo au changamoto kuyafanya maisha yawe rahisi kwa watu katika jamii".

Kisaikolojia, kunatajwa kuwapo aina mbili za watu; mtu anaye sukumwa na huduma kufanya kazi, pia anayesukumwa na mshahara kufanya kazi

• ***Mwandishi wa makala, pia ni mtuzi wa vitabu na mjasiriamali. Anapatikana kwa simu: + 255 0626 267 969***





Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Absa Tanzania, Obedi Laiser na ujumbe wake, walipomtembelea ofisini kwake, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# TCB yawaangukia wakulima kukubali makato ya 213/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BODI ya Kahawa Tanzania (TCB) imewaomba wakulima wa mikoa inayolima zao hilo kukubali makato ya Sh.213 kwa kilo kwa ajili ya kuchangia mfuko wa uendelezaji kahawa na kuchochea uzalishaji wake.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Prof. Aurelia Kamuzora alitoa ombi hilo jana jijini hapa kwenye mkutano mkuu wa 13 wa wadau wa kahawa.

Alisema kupitia fedha hizo bodi inarudisha maendeleo kwa wakulima ikiwamo kupeleka miche na kusaidia huduma za ugani.

"Niwahakikishie wakulima mchanganuo wa fedha hii ya makato tumeweka wazi na hakuna fedha itakayopotea, tuna mikakati mingi ya kuhakikisha kahawa ya Tanzania inaendelea kusifika kwa ubora wake,"alisema. Alisema Mkoa wa kagera wamekubali makato na kuwaomba wakuu wa mikoa, wilaya na wabunge kusaidia kuhamasisha wakulima wa maeneo yao kukubali.

"Tangu uhuru kahawa haijawahi kuzalishwa kwa wingi kama mwaka huu tumefikia uzalishaji wa tani 82,000 yajayo yanafurahisha na mikakati iliyopo ni kufikia tani 300,000 tunaona lengo linakwenda kutimia,"alisema.

Alisema mafanikio yaliyopatikana kutokana na mikakati ya bodi ya kukwamua zao hilo ni pamoja na kuiingizia nchi fedha za kigeni ambapo kwa msimu uliopita zao hilo liliingiza zaidi ya Dola za Marekani milioni 200.

Aliwaomba wakulima kuendelea kulima zao hilo kwa kuwa ni mali na bodi itahakikisha inatumia makato hayo kutafuta miche ili wapande zaidi.

Naye, Mratibu wa Mradi wa kuboresha na kuendeleza zao la kahawa kwa wakulima wadogo wa Nyanda za Juu Kusini kutoka Shirika la Viagroforestry, Rashid Malya, alisema shirika hilo l inatekeleza mradi wa CODE-P wa miaka minne ulianza mwaka 2020 na utahitimishwa Mei 2024.

Alisema mradi huo unalenga kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi katika mnyororo wa thamani wa zao hilo, kuongeza ajira na kuboresha usalama wa chakula na lishe kwa wakulima wadogo.

Alieleza kuwa lengo la mradi ni kufikia wakulima 24,000 katika wilaya sita za mikoa mitatu ya Mbeya, Songwe na Ruvuma ambapo hadi sasa waliofikiwa ni 21,000 huku wanaume wakitajwa kujishughulisha zaidi katika uzalishaji kuliko wanawake.

Akizungumzia kuhusu tija na uzalishaji endelevu wa kahawa aina ya robusta mkoani Kagera, mwakilishi wa Shirika la Cafe Africa, Samora Mnyaonga, alitaja vikwazo wanavyokumbana navyo wakulima kuwa ni kukosa fursa ya kupata mikopo kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa mashamba yao ya kahawa huku akitolea mfano mikopo ya pembejeo za kilimo.

# RC aziagiza h'shauri kuacha kuitumia vibaya TAKUKURU

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

HALMASHAURI za wilaya mkoani Singida zimetakiwa kuacha kuitumia vibaya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kama kichochoro kwa kuwapeleka watumishi wanaobainika kufuja fedha za mapato kwa kuwa kesi zao zinachukua muda mrefu na kuwafanya waendelee kutanua mitaani.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba aliyasema hayo jana kwenye kikao maalum cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Manyoni cha kupitia hoja za ukaguzi zilizoibuliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Hatua ya kueleza hayo ilifuatia baada ya kubainika kuwa Sh.milioni 18 zilizokusanywa na watendaji kwa mashine ya POS hazikupelekwa benki.

Alisema tatuzo hilo pia lilijitokeza katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ambapo Sh.milioni 118 zilizokusanywa hazikupelekwa benki.

"Nimetembea halmashauri zote za Mkoa wa Singida, mnaitumia vibaya TAKUKURU watu wanaiba halafu wanapelekwa TAKUKURU tu wakati wapo waliowadhamini, benki ukikopa ukiweka dhamana hawahangaiki na wewe wanahangaika na dhamana lakini ninyi mnakimbilia haraka TAKUKURU na kuwaachia waliowadhamini," alisema.

Serukamba alisema kuanzia sasa iwe diwani au mtumishi yeyote kama alimdhamini mkusanyaji mapato waliomdhamini wabanwe na kulipa fedha za serikali hata kama ni kwa kuuza nyumba yake ili kukomesha tabia hiyo.

Alisema haiwezekani mtu anaiba halafu anapelekwa haraka TAKUKURU ambako anajua kesi itachukua muda mrefu na kumfanya aendelee na biashara zake huku halmashauri ikikosa mapato.

"DED (Mkurugenzi) wewe ni mgeni naomba uwe mkali, halmashauri hii ya Manyoni lazima uingie ukiwa unajua lazima uwe rafu, hawa watendaji wanatufanyia mambo ya hivyo kabisa," alisema.

Aidha, alionya halmashauri kuacha tabia ya kufanya usuluhishi kwa watu wanaobainika kufuja fedha za mapato badala yake hatua kali ziwe zinachukuliwa kwa mujibu wa sheria.

Naye, Katibu Tawala Mkoa wa Singida Dk. Fatuma Mganga, alisema kama wanaofuja fedha za mapato ni watumishi kuna haja gani ya kumpeleka TAKUKURU wakati anaweza kubanwa kwa kutumia sheria za kiutumishi akalipa fedha hizo hata kama ni kwa kumkata kwenye mshahara wake.

"Kama ni mtendaji tunafahamu amekusanya Sh.milioni tano lakini amepeleka benki Sh.milioni mbili na Sh.milioni tatu amebaki nazo huyu tunampeleka TAKUKURU kufanya nini badala ya kumbana alipe hizo fedha vitu vyake vinataifishwa vinauzwa tunapata pesa yetu," alisema.

Dk.Mganga alisema hivi sasa imekuwa kama 'fashion' ama uchocholo kwa wanaofuja fedha za Serikali kupelekwa TAKUKURU na kwamba imefika wakati kubadilisha mbinu za kudai fedha kwa kuwabana ikiwamo ni kuuza vitu vyao ili kurejeshwa fedha za serikali.

# Serikali yaendelea mapambano kukabiliana maafa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imesema inaendelea kuboresha mikakati ya kukabiliana na maafa ili kuhakikisha wananchi wanaishi katika hali ya usalama.

Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia utafiti wa maafa Idara ya Menejimenti ya Maafa wa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Charles Msangi, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha wataalam waliokutana kwa lengo la kufanya tathimini ya uwezo wa kukabiliana na maafa.

Msangi alisema nchi imepiga hatua kubwa katika kukabiliana na maafa kutokana na kuimarisha mfumo wa utendaji kwa kutunga Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Na. 6 ya mwaka 2022 na kanuni zake za mwaka 2022 ya kuimarisha mifumo ya tahadhari ya mapema na miundombinu, vifaa na miongozo kwa ajili ya kukabilina na maafa na kurejesha hali.

"Nchi imepiga hatua katika kutekeleza mkakati wa Sendai kwa kuweka mazingira ya uwekezaji katika kupunguza vihatarishi vya maafa kwa kuandaa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa (2022-2027) pamoja miongozo, mipango na mikakati ya kitaifa na kisekta," alisema

Mkurugenzi huyo alisema kila sekta inapaswa kuwa imara katika eneo lake, ili kuepuka madhara kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kulingana na uwezo uliopo sasa wa kukabiliana na maafa hivyo akawasisitiza wataalam kuzielewa kabla ya kuchukua hatua yoyote. "Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa iliratibu zoezi la tathmini ya uwezo wa udhibiti wa maafa kupitia jumuiya ya ushirikiano inayotambulika kama Capacity for Disaster Reduction Initiative (CADRI) inayojumuisha mashirika 20 ya Umoja wa Mataifa na kimataifa yanayotoa huduma za kibinadamu na kutekeleza shughuli za maendeleo,"alisema.

Alisema tathmini ilifanyika kuanzia Oktoba 17 hadi 28 mwaka jana ikilenga kutambua hali ya uwezo uliopo na maeneo ambayo mashirika husika yanaweza kushirikiana na serikali kuimarisha udhibiti wa maafa nchini.

Naye, Naibu Mkurugenzi Mkaazi kutoka WFP, Brian Bogart aliishukuru serikali kwa kushirikiana na shirika hilo ili kuhakikisha raia wake wanashiriki katika shughuli za maendeleo wakiwa katika mazingira rafiki.



## HABARI MBEYA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (wa pili kushoto), akizungumza na wataalamu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mkoa wa Ruvuma walipotembelea mgodi wa makaa ya mawe wa Jitegemee, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Taharuki yazuka, lori la mafuta likilipuka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALI ya taharuki ilitanda juzi jijini Mbeya baada ya lori la mafuta lililokuwa likichomelewa na mafundi kwenye kituo cha mafuta cha Infinity kilichopo eneo la Mafiati kulipuka na kutoa kishindo kilichozua hofu.

Aidha, katika tukio hilo watu wawili ambao ni miongoni mwa waliokuwa wanachomelea tangi walijeruhiwa na kukimbizwa hospitalini kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

Kishindo cha lori hilo ambacho kilikuwa mithiri ya bomu kilisikika katika maeneo mbalimbali ya Jiji hilo ambapo shughuli zilisimama kwa muda kutokana na hofu. Mfuniko wa tangi hilo lililokuwa likichomelewa uliruka juu umbali wa zaidi ya mita 100 na kwenda kuparamia lori lingine ambalo lilikuwa likisubiri taa za kuongozea magari ziwake ili liendelee na safari.

Hata hivyo lori hilo lilizua hofu zaidi baada ya kuwaka moto ambao ulidhibitiwa na maofisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kabla haujasababisha madhara makubwa.

Meneja wa Kituo cha Mafuta cha Infinity, Fredrick Donald alisema lori hilo lilikuwa limebeba mafuta aina ya dizeli lakini lilikuwa na ufa mdogo uliokuwa unasababisha mafuta kuvuja.

Alisema baada ya kutoa mafuta mafundi waliamua kulichunguza ili kubaini ufa huo na kuuziba na kwamba walipouona ndipo walianza kuchomelea kabla ya kwenda kujaza tena mafuta.

"Lilikuwa limejaa gesi ndani iliyosababisha kufumuka, lakini tunashukuru halijaleta madhara makubwa sana, wamejeruhiwa mafundi wetu wawili ambao ni Ally Mshana na Eric Samwel. Tumewapeleka hospitalini na wanaendelea vizuri," alisema Fredrick.

Alilishukuru Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kuwahi kuudhibiti moto uliokuwa unawaka kwa maelezo kuwa wangechelewa ungesababisha maafa zaidi.

Baadhi ya mashuhuda walisema baada ya kusikia kishindo hicho waliamua kufunga shughuli zao kwa muda ili kufuatilia kwanza kilichokuwa kimetokea.

Mmoja wa wananchi hao, Kemia Mwakalinga alisema anafanya shughuli zake karibu na kituo hicho na aliposikia kishindo alifunga na kwenda kuangalia kilichokuwa kimetokea.

Alisema alishuhudia watu wawili wakiwa wamelala chini baada ya kujeruhiwa huku tangi la mafuta walilokuwa wakichomelea likiwa linawaka moto.

Alisema tangi hilo lingekuwa na mafuta madhara yangekuwa makubwa zaidi kutokana eneo hilo kuwa na magari mengi ambayo baadhi yalikuwa yameegeshwa na mengine yalikuwa barabarani.

"Kwahiyo tumewachukua majeruhi na kuwakimbiza hospitalini japokuwa mpaka sasa hatujui hali zao, lakini hili tukio limetushtua kwa sababu halijawahi kutokea," alisema Mwakalinga.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mbeya, Gervas Fungamali alisema kwa kawaida tangi la mafuta hata kama mafuta yatakuwa yameondolewa huwa gesi inakuwemo.

Alisema gesi hiyo ndiyo iliyosababisha mlipuko huo na kwamba walipofuatilia walibaini kuwa madhara yalikuwa madogo endapo lingekuwa na mafuta.

Aliwataka wafanyakazi wa magari hayo kuwa makini wanaposhughulikia mivujo ya mafuta kwenye vyombo hivyo kwa maelezo kuwa ni hatari kwa maisha yao. Aliwataka wananchi kutoa taarifa mapema kwa jeshi hilo linapotokea tatizo la aina hiyo ili kupunguza madhara kama ambayo walifanya kwenye tukio hilo.

# Serikali yatoa bil.75/- utekelezaji miradi 6 umwagiliaji

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI kupitia Wizara ya Kilimo imetoa Sh. bilioni 75 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi sita ya umwagiliaji katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila aliyasema hayo juzi wakati wa ukaguzi wa mradi wa umwagiliaji wa Uturo-Isenyela uliopo katika Kata ya Mapogoro wilayani humo.

Mradi huo ili ni miongoni mwa maeneo ambayo skimu zake zinaboreshwa ili kuwasaidia wakulima kuondokana na kero ya mazao yao kukauka kwa kukosa maji.

Alisema skimu hiyo ya Uturo-Isenyela inajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 14 na kwamba ikikamilika itakuwa ni suluhisho la tatizo la wananchi kugombea maji.

"Miradi mingine ya umwagiliaji tuliyopatiwa fedha ni mradi wa Chasiheiman ambao tumepewa Sh. bilioni 15, Matebele-Gonakuvagololo Sh.bilioni 10, Msesule Sh. bilioni 13, Madibira Sh.bilioni tisa na mradi wa Mbuyuni mpaka Makengelewe wenye thamani ya Sh. bilioni 14," alisema Kanali Mwila.

Alisema yeye pamoja na wasaidizi wake watahakikisha wanasimamia kwa ukaribu ili kuhakikisha miradi yote inakamilika kwa wakati na kuleta tija ambayo inakusudiwa.

# Jafo aagiza migodi kuzingatia uhifadhi mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** RUVUMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ameagiza migodi yote nchini kuhakikisha ina mpango mkakati wa kurejesha mazingira kwenye hali yake ya zamani baada ya shughuli za uchimbaji kumalizika.

Waziri jafo alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea machimbo ya migodi ya Jitegemee, Tancoal na Ruvuma Coal iliyoko mkoani Ruvuma, kuangalia namna inavyotunza mazingira.

Alisema TANCOAL ilisimamisha uzalishaji kwa muda lakini amefurahi kuona umeanza shughuli za uzalishaji na wamekuwa wakitunza mazingira kwa kurejesha maeneo waliyochimba.

Alisema pia amefurahi kuona kampuni ya uchimbaji ya Ruvuma Coal imefanya uwekezaji mkubwa na kwa sasa umepata uwezo wa kuzalisha tani 200,000 za makaa ya mawe kwa mwezi.

Alisema amefarijika pia kuona migodi hiyo inachimba makaa ya mawe lakini inazingatia mazingira kwa kurejesha udongo sehemu zote wanapochimba madini hayo.

"Nimewataka wawekezaji wengine kwenye migodi yote nchini wahakikishe wanapochimba rasilimali madini wanarejesha mazingira vizuri na wakitaka kujifunza waje huku Wilaya ya Mbinga Ruvuma wataona wenzao wanavyofanya," alisema

Aliongeza: "Nimemwelekeza Mkurugenzi wa NEMC atembelee migodi yote hasa ya Kanda ya Ziwa ili wale wote wanaochimba madini lakini hawarejeshi ardhi iliyoharibiwa kwenye hali yake ya zamani wafanye hivyo haraka kabla ya kuchukuliwa hatua," alisema Waziri Jafo.

Alisema wachimbaji wengi wanatumia madini ya sulphur wakati wa shughuli za uchimbaji, hivyo wanapaswa kudhibiti utirishaji wa maji yanayotoka kwenye migodi yao.

"Nimetoa maelekezo wadhibiti utiririshaji wa maji ambayo yanaweza kuleta athari kwenye maisha ya binadamu lakini pia nimefurahi maeneo yote niliyotembelea na wameshaonyesha utayari wa kutunza mazingira," alisema.

Kuhusu usafirishaji wa makaa ya mawe, Waziri Jafo aliwataka wamiliki wa malori yanayosafirisha wayafunike makaa hayo ili yasilete athari kwa maisha ya binadamu yanapokuwa yakisafirishwa.

Alisema NEMC ni baraza ambalo limeundwa kwa mujibu wa sheria kusimamia mazingira hivyo wajibu wao ni kulinda mazingira na watu wanapowaona wakitekeleza majukumu yao wawape ushirikiano wa kutosha.

Alisema popote NEMC inapoonekana iko kwa ajili ya kusimamia sheria ya mazingira hivyo watu wanapaswa kutii sheria badala ya kuinyooshea kidole na kuishambulia.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyosababisha kuongezeka kwa migodi ya makaa ya mawe.

Alisema zamani kulikuwa na mgodi mmoja tu wa makaa ya mawe wa Kiwira lakini kwa sasa kumetokea fursa za migodi mikubwa inayochimbwa makaa ya mawe ambayo inatia hamasa kwamba nchi inakwenda kwa kasi kwenye migodi.

# Asilimia 46 ya magari Zanzibar hayajakatiwa bima

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MENEJA wa Shirika la Bima Tanzania (TIZA) Ofisi za Zanzibar, Mohamed Khamis Amer, amesema asilimia 46 ya magari visiwani Zanzibar hayajakatiwa bima.

Amesema kuna haja ya kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili wakate bima, kupata fidia wanapokutwa na majanga ikiwamo ajali. Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari visiwaini Zanzibar kuhusu uhamasishaji jamii na umuhimu wa ukataji wa bima.

Alisema kwa mujibu wa takwimu kutoka Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) magari yaliongia Zanzibar na kusajiliwa mwaka 2022 ni 265,000 na asilimia 54 ndiyo yaliokatiwa bima.

Meneja huyo alisema kwa mujibu wa sheria kila ajali inayotokea barabarani lazima ilipwe fidia na fidia hiyo italipwa mara ya kubainika kuwa kuna mkataba wa bima.

"Ni wajibu wa kila mtumiaji wa chombo cha moto kukata bima na anapokua na bima anapopata ajali badala ya yeye kudaiwa fidia ya kumlipa mwathirika jukumu hilo linahamia kwenye kampuni ya bima"alisema

Alisema suala hilo linamaslahi kwa mtumiaji wa chombo, mtumiaji wa barabara na taifa kwa ujumla, hivyo wananchi ni nguvu kazi ya taifa na uwepo wao ni muhimu kwa serikali.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Msaraka, alisema bado watumiaji wengi wa vyombo vya moto hawatii sheria ya ukataji wa bima mpaka washurutishwe.

Alisema ni marufuku kwa chombo cha moto kutembea katika wilaya yake bila ya kuwa na bima, kwamba ka yeyote atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Haipendezi kukamatana kama tunafukuza mwizi...... hakikisha unakata bima yako na uendeshe chombo chako bila ya kushurutishwa, "alisema.

Aidha alisema kuna changamoto ya kutoheshimiwa kwa sheria zilizopo na kuna tatizo la kuoneana muhali katika utekelezaji wa sheria hizo wakati kutokata bima ni kosa la kisheria.

Hivyo, aliwataka wasimamizi wa sheria ikiwemo Jeshi la Polisi kutomuonea huruma mtu yoyoyte atakaekamatwa anaendesha chombo cha moto bila ya kuwa na bima.

Alisema serikali kwa kushirikiana na mamlaka ya bima itafanya opereshen maalum ya kukagua vyombo vyote vya moto vitavyotembea katika wilaya hiyo ambayo itaanza Juni 25 mwaka huu.

Naye Mkurugenzi wa TIRA Zanzibar, Khadija Said, alisema lengo la kuwashurutisha wananchi kutii sheria bila ya shuruti katika ukataji wa bima ni kuongeza ukusanyaji wa mapato ya serikali.



Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Serikali: Tumeweka mazingira mazuri kwa wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imeweka mazingira mazuri kwa wawekezaji katika miradi ya uwekezaji ikiwemo kuhusisha misamaha ya ulipaji wa kodi.

Hayo yalisemwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga wakati akijibu swali la mwakilishi wa Wawi, Bakari Hamad Bakari, aliyetaka kujua mazingira gani yamewekwa na Zanzibar katika kuwavutia wawekezaji.

Akijibu swali hilo, Waziri Soraga alisema ipo misamaha ya kodi mbalimbali huku akitolea mfano wa kodi ya uingizaji wa bidhaa pamoja na usafirishaji wa nje.

Alizitaja faida nyingine ikiwemo ruhusa ya kutumia makandarasi wa nje katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ikiwemo ya ujenzi pamoja na ajira kwa wageni.

Alisema kwa sasa Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu katika maeneo huru ya uchumi yaliopo Fumba kwa Unguja na Micheweni kwa Pemba ili fursa hizo ziweze kutumiwa na wageni.

Waziri Soraga alisema katika maeneo huru ya Micheweni huko Pemba tayari ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita saba ipo katika hatua za mwisho kukamilika na hivyo kukifungua Kisiwa cha Pemba katika uwekezaji wa miradi ya kimkakati.

Aidha, alisema huduma za miundombinu mingine tayari zimefikishwa ikiwamo maji safi na salama pamoja na huduma ya nishati ya umeme kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya viwanda.

Alisema: "Mheshimiwa hiyo ndiyo mikakati na faida zinazopatikana katika uwekezaji kwa wageni ambapo kwa sasa tupo katika hatua za mwisho za ujenzi wa miundombinu katika maeneo huru ya uwekezaji yaliopo Fumba pamoja na Micheweni kwa upande wa Pemba".

# Serikali kuifungua Zanzibar ukanda Afrika, duniani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema serikali imedhamiria kuifungua Zanzibar katika Ukanda wa Afrika na duniani kwa kuwaalika wawekezaji.

Alisema sekta kuu inayotegemewa ni sekta ya utalii, kwamba asilimia 40 ya uwekezaji wote upo katika sekta hiyo, hivyo wanasheria wanasehemu kubwa ya kusaidiana na serikali katika kufikia azma na malengo yake.

Aliyasema hayo viswani Zanzibar mwishoni mwa wiki wakati akifungua mkutano mkuu wa Jumuiya ya Mawakili Zanzibar ulioambana na uchaguzi mkuu wa jumuiya hiyo.

Alisema wanasheria wanalalamikiwa katika utoaji wa huduma mbovu kwa wawekezaji hivyo ni vyema kufahamu tofauti kati ya mwanasheria anapotoa huduma na mteja wake anaemhudumia.

"Wateja wenu wanapowatafuta kwanza simu hamuwapokelei, mnasema ananikera sana, simu hazishi lakini mimi ndiyo niliyekupa kazi ninakila haki ya kukutafuta muda wote wa kupata taarifa ya kazi yangu," alisema.

Soraga alisema taarifa zao zimeshafika serikali, hivyo hawapaswi kuwa wakali kwa wateja wao kwa sababu wanawategemea wao katika kutoa huduma.

Aidha, aliwataka kujifunza namna ya kutoa huduma kwa mteja hasa katika kutumia lugha nzuri ambayo haitomuuzi mteja.

Waziri Soraga aliwataka wanasheria na mawakili hao kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufanikisha maendeleo ya kiuchumi na kuacha majungu baina yao.

Naye, Slim Abdallah Said, aliyewahi kuwa rais wa jumuiya hiyo alisema wanasheria ni kiungo muhimu katika nyororo wa thamani ya uwekezaji na husimamia haki, kuhakikisha sheria zinazingatiwa na kwa maana hiyo kama hakuna wanasheria hakuna uwekezaji.

Alisema mazingira yenye utulivu wa kisheria ndio yenye kuchochea uwekezaji endelevu pamoja na ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

3 FORM 58
IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 581 OF 2023
In the Matter of the Estate of the Late
LAWRENCE SHELUKINDO SAGUTI
And
In the Matter of Application for letters of administration
by
GRACE SAGUTI JENGO
GENERAL CITATION
(Rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 4 day of 7, 2023.

**Dated at DAR ES SALAAM this 16 day of 6, 2023.**

Senior Resident Magistrate

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Temeke
Kituo cha Jumuishi Mkoa Dar es Salaam
Usimamizi wa mirathi Na.885/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU Idrisa Kassim Chande WA Lindi
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA
NA Aboud Kassim Chande
TANGAZO
(kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi
Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 mwezi 7 Mwaka 2023 kabla huyo mwombwji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo Tarehe 15 mwezi 06 mwaka 2023**

---

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
IN THE DISTRICT COURT OF ARUSHA
AT ARUSHA
CIVIL/APPLICATION/CASE/NO 13 OF 2023
AGRIMATCO TANZANIA LTD..... PLAINTIFF
VERSUS
HAROUN SANGILE DEFENDANT/RESPONDENT/-J/DEBTOR

NOTICE OF JUDGMENT

**TO: HAROUN SANGILE**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **JUDGEMENT** in the District Magistrate's Court of Arusha at Arusha on the **30th day of JUNE 2023 at 09:00 O'clock** in the forenoon.

You may appeal in person or by Advocate or agent duly authorised to appeal on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE:** That in default of your appearance on that day time before mention or hearing the Court may proceed in your absence.

**GIVEN under my hand and Seal of the court this 21st day of JUNE 2023.**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
Probate and Administration Cause No. 62 of 2023
In the matter of the Estate of the late
GERALD AMOS MSANJA Of CHIDACHI
within Dodoma Region
And
In the matter of the application for letters of administration by CHARLES MSANJA AMOS
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **3 Day of JULY, 2023**

**Date at Dodoma this 22 day of MAY, 2023.**

PETITIONER

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
Probate and Administration Cause No. 72 of 2023
In the matter of the Estate of the late
SAMSON HITLA DANIEL MANGASIN of KIKUYU MISSION
within Dodoma Region
And
In the matter of the application for letters of administration by
MERKIZEDEKI SAMSON MANGASIN

GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **24 Day of 7, 2023**

**Date at Dodoma this 15 day of JUNE, 2023.**

PETITIONER

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHARLES KULEBE MAKOBA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI AINA YA LANDROVER YENYE USAJILI NAMBA **T 598 ABH** KWA YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/212742/2023**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO
TANGAZO LA KUITWA SHAURINI
SHAURI LA MADAI NAMBA 29, 2023

MDAI: DENIS LUWANDA
DHIDI
MDAIWA: GIBSON ZABLON BUZOYA

**KWA:GIBSON ZABLON BUZOYA**
**DAR ES SALAAM**

**Ombi la mdai:DENIS LUWANDA**
**Madai ya MADAI YA PESA TSH. 220,000/=**
Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limapangwa kusikilizwa mnamo tarehe 26 Mwezi 6 Mwaka 2023 Saa 2:30 Asubuhi/alasiri.
Angalia kama hukuhudhuria / hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 20 mwezi 6, 2023**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI, MOROGORO.


***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Kitendawili matajiri waliopotea na Titan

**WASHINGTON,** Marekani

SAFARI ya matajiri waliolipa dola 250,000 sawa na Sh. milioni 600 kwa kila mmoja kwa ajili ya kwenda kutalii mabaki ya meli ya Titanic kwa kutumia nyambizi ya Titan iliyopotea Jumapili, imeendelea kuingia mashakani baada ya muda wa hewa ya ziada inayowawezesha kupumua kuisha.

Kwa mujibu wa walinzi wa pwani ya Marekani matajiri hao wanne walikuwa na saa 30 pekee za kupata hewa ya oksijeni inayowawezesha kupumua ambayo ilibaki katika chombo hicho, muda ambao umeisha rasmi jana licha ya kwamba nyambizi hiyo bado haijapatikana.

Wataalamu wanasema muda wa kuelekea kuisha kwa hewa ya oksijeni ni wa kinadharia zaidi, kwa kuzingatia kwamba chombo hicho kilichopotea kinaweza kuwa bado kiko katika hali nzuri na hakijanasa au kuharibiwa katika kina kirefu au karibu na sakafu ya bahari.

**Hilo halikufanyika kwahivyo lazima niamini kwamba kutokana na ushahidi, ilibidi iwe sio tu kushindwa kwa mawasiliano, lakini aina fulani ya kushindwa kwa jumla kutokana na janga.**

Aidha, inaelezwa kuwa waokoaji wanaoitafuta nyambizi hiyo wameongeza juhudi zaidi kwa kueleekeza nguvu zao katika eneo la mbali la Atlantiki sehemu kelele za chini ya bahari zilipogunduliwa, huku maofisa wakitahadharisha juu ya kuweka matumaini makubwa ya kuipata.

Inaelezwa kuwa nyambizi hiyo yenye urefu wa mita 6.7 inaendeshwa na kampuni ya usafirishaji ya OceanGate ya nchini Marekani, ambayo ilianza safari yake ya kuzama chini ya bahari Jumapili asubuhi kwa saa za Marekani.

Kikosi cha ulinzi wa pwani cha Marekani kilisema vyombo vya utafutaji vinavyoendeshwa kwa rimoti vilipelekwa chini ya bahari karibu na mahala ambako ndege ya Canada ilirekodi sauti kwa kutumia mfumo wa vinasa sauti wa sonar juzi, na kwamba havipati ishara yoyote ya nyambizi hiyo ya utalii.

Inaelezwa kuwa timu za uokozi kutoka Marekani, Canada na Ufaransa zinatumia ndege na meli kutafuta eneo la wazi la bahari lenye ukubwa wa maili 10,000 za mraba, kutafuta nyambizi hiyo.

Inabainishwa kuwa nyambizi hiyo ilipoteza mawasiliano na meli yake ya msaada karibu na mwisho wa umbali iliyopaswa kusafari kwa saa mbili kutazama mabaki ya meli ya Titanic.

Dk. Michael Guillen, mwanasayansi ambaye alinusurika ajali wakati wa safari ya kwenda kwenye mabaki ya Titanic mwaka 2000, alisema uelewa wake ni kwamba Titan iliundwa katika mfumo ambao inapokutana na shida ungeiwezesha kuwa na vifaa vya kuelea hadi kwenye uso wa bahari.

"Hilo halikufanyika kwahivyo lazima niamini kwamba kutokana na ushahidi, ilibidi iwe sio tu kushindwa kwa mawasiliano, lakini aina fulani ya kushindwa kwa jumla kutokana na janga," alisema.

Katika kuimarisha juhudi za utafutaji wa nyambizi hiyo, meli ya utafutaji wa Ufaransa ya Atalante, ilitumwa kupeleka chombo cha roboti chenye uwezo wa kushuka kwenye kina cha mbali kupita yalipo mabaki ya meli ya Titanic kwa maili mbili.

Roboti hiyo inayoweza kutazama chini ya maji ya Ufaransa, iliyopewa jina la Victor 6,000, ilitumwa kwa ombi la kikosi cha jeshi la majini la Marekani, ambacho pia kilituma mfumo wake maalum wa uokoaji uliyoundwa kuinua vitu vikubwa, na vizito chini ya bahari kama vile ndege iliyozama au meli ndogondogo.

Watu waliomo kwenye safari ya nyambizi hiyo ni Bilionea wa Uingereza na mzinduzi Harmish Harding mwenye umri wa miaka 58, mfanyabiashara mzaliwa wa Pakistan Shahzada Dawood mwenye miaka 48 na mtoto wake wa kiume Suleman, ambao wote ni raia wa Uingereza.

Mgunduzi wa Ufaransa Paul-Henri Nargeolet mwenye umri wa miaka 77, na Stockton Rush, Mwanzilishi na mtendaji mkuu wa OceanGate, pia walikuwamo ndani ya nyambizi hiyo. **DW**

## Mikakati kusaidia nchi masikini yatangazwa

**PARIS,** Ufaransa

MKUU wa Benki ya Dunia ametangaza hatua kadhaa za kusaidia nchi zinazokumbwa na majanga ya asili, ikiwemo kusitishwa kwa muda wa ulipaji wa deni kwa wakopeshaji, wakati viongozi wa dunia wanakutana mjini Paris ili kutoa msukumo wa agenda mpya ya fedha duniani.

Viongozi 40, wakiwemo zaidi ya 10 kutoka Afrika, waziri mkuu wa China na Rais wa Brazil, wamekutana katika mji mkuu wa Ufaransa na mashirika ya kimataifa kwenye mkutano kujadili kuhusu mkataba mpya wa kifedha duniani na mabadiliko ya hali ya hewa.

Ilielezwa kuwa mkutano huo unalenga kuongeza ufadhili kwa nchi zenye kipato cha chini, kufanya mageuzi kwenye mifumo ya kifedha ya baada ya vita na kutoa fedha za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Pia ilielezwa kuwa jitihada hizo zinalenga kufikia maridhiano ya ngazi ya juu kuhusu jinsi ya kuendeleza mipango kadhaa ambayo kwa sasa inakabiliwa na changamoto kama ile ya kundi la nchi zilizoendelea kiuchumi (G20), kongamano la mazingira (COP), IMF, Benki ya Dunia na Umoja wa Mataifa (UN). **VOA**

**Viongozi 40, wakiwamo zaidi ya 10 kutoka Afrika wamekutana katika mji mkuu wa Ufaransa kwenye mkutano kujadili kuhusu mkataba mpya wa kifedha.**




Meli ya utafiti na utafutaji ya Ufaransa, Atalante, iliyotumwa kupeleka chombo cha roboti kinachoweza kuzama mbali ilipo meli ya Titanic katika juhudi za kutafuta nyambizi ya Titan. **PICHA: MTANDAO**

## Airtel kuzindua intaneti 5G Tz

**LAGOSI,** Nigeria

KAMPUNI ya Airtel Afrika, imezindua mchakato wa kuhamia masafa ya mtandao wa 5G nchini Nigeria, ili kutoa huduma za kisasa na kasi kwa wateja wake huku ikieleza nia ya kufanya hivyo Tanzania hivi karibuni.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na kampuni hiyo uzinduzi wa masafa hayo ya mtandao wa 5G utafanyika awali katika nchi tatu ikianzia Nigeria, Tanzania na Zambia, na kwamba mipango ya kusambaza maeneo yaliyobaki kwenye soko zima inaandaliwa.

Ilisema kwa kutumia mtandao wa 5G, wateja wao wataweza kufurahia kuangalia video zikiwa angavu zaidi ya ilivyo sasa, kufurahia kutazama michezo mtandaoni, kurusha matukio mubashara pamoja na kupata kasi ya mtandao wakiwa popote.

"Kutokana na kwamba wigo wa mawasiliano utapanuka zaidi kutokana na teknolojia ya kisasa ya 5G pia shughuli za biashara zitaimarika hasa zinazotumia mtandao kutoa huduma zake, pamoja na kufanikisha mikutano ya mbali mubashara kupitia mtandao," ilisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel Afrika, Segun Ogunsanya alisema kupitia mtandao wa 5G, watawapa wateja wao fursa ya kuishi kidijitali kwa kufurahia huduma ya teknolojia itakayotolewa na mtandao huo.

"Kwa kukamilisha hili kwa nchi zetu hizi tatu ikiwemo Tanzania tunadhihirisha dhamira yetu tuliyojiwekea ya kuwekeza katika teknolojia ya mtandaoni ya kisasa zaidi, ili kufungua wigo mpana na kutoa fursa kwa watumiaji, tunawezesha kuiunganisha dunia kidijitali pamoja na wateja wetu kukamilisha maono waliyonayo," alisema Ogunsanya.

Aliongeza kuwa mtandao wa 5G utajikita zaidi katika maeneo maalum ikiwemo makazi yenye msongamano mkubwa wa watu na yale yenye huduma kama maduka, hospitali, katikati ya miji na maeneo makuu ya kibiashara.

# KAZE KWENYE RADA ZA GEITA GOLD FC

**Na Saada Akida**

BAADA ya Uongozi wa Geita Gold kutangaza kuachana na kocha wao Fredy Minziro inadaiwa sasa wanamuwinda kocha msaidizi wa Yanga, Cedrick Kaze ili kumpa kazi ya kufundisha timu hiyo msimu ujao.

**Kaze raia wa Burundi alitangaza kumaliza mkataba wake kuitumikia Yanga mara baada ya kumalizika kwa msimu uliopita.**

Inaelezwa Kaze anapewa nafasi kubwa ya kupewa mikoba ya kuifundisha timu hiyo kutokana na kufanya kwake vizuri akiwa na kikosi cha Yanga.

Mmoja wa viongozi wa Geita Gold FC, aliiambia Nipashe kuna asilimia kubwa ya Kaze kupewa jukumu la kuwa kocha mkuu ndani ya kikosi cha timu hiyo kwa sababu ya mafanikio waliyoyapata Yanga kwa msimu uliomalizika wa 2022/23.

"Kaze ndio jina ambalo liko mezani kwa viongozi na kutajwa sana kuwa atakuja kuchukuwa nafasi ya Minziro, hadi sasa kocha huyo bado hajasaini mkataba mwingine na Yanga, uongozi utapeleka ofa kwake na kuona uwezekano wa kuwa naye msimu ujao," alisema kiongozi huyo.

Alisema kuna maboresho ambayo uongozi wa klabu hiyo umepanga kuyafanya kabla ya kuanza msimu mpya na maeneo wanayoyaangazia ni kuwa na benchi bora la ufundi pamoja na kuongeza wachezaji wengine wenye ubora.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Leonard Bugomora alipotafutwa kuzungumzia mipango hiyo alisema "kwa sasa siwezi kumzungumzia jambo lolote kwa sababu nipo katika majukumu makubwa, labda muwasiliane na Katibu wetu," alisema Bugomora.

Geita Gold FC ilimaliza ligi kwenye nafasi ya saba na msimu uliopita na msimu ujao imepania kufanya makubwa.






Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Buza, wakifanya mazoezi ya mpira wa Magongo katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mubiru: Ninamatumaini kushinda 'Play Off'

**Na Abdallah Mataka**

KOCHA wa Mbeya City, Abdallah Mubiru amesema kutokana na maandalizi waliyoyafanya kuelekea kwenye mchezo wao wa marudiano wa mchujo 'Play Off' dhidi ya Mashujaa FC, ana matumaini makubwa ya kuibuka na ushindi.

Mchezo huo ambao awali ulipangwa kuchezwa jana kwenye uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, sasa utachezwa kesho kwenye Uwanja huo.

Mashujaa wataingia uwanjani wakiwa mbele kwa mabao 3-1 kutokana na ushindi walioupata kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa Uwanja wa Tanganyika mjini Kigoma.

Mubiru alisema tayari wamefanyia kazi mapungufu waliyoyaona kwenye mchezo uliopita na wamewasoma vizuri wapinzani wao ambao walikuwa wageni kwao kwenye mchezo wa kwanza.

"Nina imani kubwa kuelekea mchezo wetu wa marudiano, tumeona ubora wa wapinzani wetu, makosa ambayo tuliyoyafanya kwenye mchezo wa kwanza tumeyafanyia kazi, tumejiandaa vizuri na tutatumia faida ya kucheza nyumbani kupata ushindi mzuri utakaotubakisha ligi kuu," alisema Mubiru.

Alisema mojpa ya sababu ya kupoteza mchezo wao wa kwanza ni uchovu kwa wachezaji wake kutokana na kucheza mechi za mfululizo.



"Uchovu ulichangia, lakini kwenye mchezo wa kesho hatutakuwa na Abdulrazaki Hamza ana matatizo ya kifamilia na Richardson Ng'ondya bado tutaendelea kumkosa ana matatizo ya kiafya, pamoja na yote bado ninao wachezaji wa kunipa ushindi kwenye mchezo huu," alisema Mubiru.

"Naweza kusema tunajiamini,wachezaji wote wameahidi kufanya kazi nzuri huku wakijua kwamba ni 'last chance'ya mwisho kubaki kwenye ligi hivyo ni suala la kusubili mechi ifike"alisema .

Katika mchezo huo wa kesho, Mbeya City inahitaji ushindi wa kuanzia mbaoa 2-0 kuweza kubakia ligi kuu, kinyume na matokeo hayo itashuka daraja na kuwapa nafasi Mashujaa kupanda Ligi kuu.

## 'Run for Binti Marathon 2023' kufanyika Julai 2

**Na Frank Monyo**

MBIO za Marathoni zilizopewa jina la 'Run For Binti' kwa mwaka huu zimepangwa kufanyika Julai 2 jijini Dar es Salaam zikiwa na lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya kuwawezesha watoto wa kike kupata taulo za kike.

Mbio hizo ambazo awali zilikuwa zifanyike Julai 30 na kurudishwa nyuma, zinaandaliwa na Shirika la sheria la ' Legal Services Facility' (LSF) kwa kushirikiana na Shirika la Smile for Community (S4C) ambapo zaidi ya washiriki 1,500 watashiriki.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa S4C, Flora Njelekela alisema mbali na mabadiliko ya tarehe za mbio hizo, LSF na S4C wanayofuraha pia kuzindua jezi mpya kwa ajili ya mbio zilizobuniwa kwa ubora mzuri na kumfanya mshiriki ajisikie amani wakati wote wa mbio.

Aidha aliitaja mikoa ambayo itanufaika na mbio hizo kuwa ni Mtwara na Lindi, ambapo watoto wa kike kwenye shule za sekondari watapatiwa bidhaa za hedhi salama na uboreshwaji wa miundombinu hususani vyoo salama.

## Mtibwa yaanza kwa kishindo Ligi ya TFF U-20

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi ya Vijana chinia ya miaka 20, Mtibwa Sugar, imeanza kwa kishindo ligi hiyo kwenye Uwanja wa Azam Complex baada ya kupata ushindi mnono wa mabao 5-0 kwenye mchezo wao wa kwanza dhidi ya Mbeya City.

Mabao ya washindi yalifungwa na Ezekiel Eusebio na Said Mkopi kila mmoja akifunga mabao mawili na Athumani Makambo aliyefunga bao moja. Mtibwa Sugar imeanza kuonyesha mapema makali yake kama ilivyokuwa msimu uliopita waliotwaa ubinmgwa wa michuano hiyo.

Katika michezo mingine ya ufunguzi wa ligi hiyo ya vijana Ruvu Shooting ilishinda mabao 3-1 dhidi ya Namungo, Geita Gold ilipata ushindi wa mabao 2-0 mbele ya KMCikaingia uwanjani na kuichakaza KMC na Coastal Union ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Singida Fountain Gate.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara la Habari na Mawasiliano ya Shirikisho la soka Tanzania (TFF), ligi hiyo inaendeshwa kwa mtindo wa makundi, kila kundi likiwa na timu nne na itachezwa hadi Juni 26 na baada ya hapo itaingia kwenye hatua ya robo fainali itakayoanza Juni 28 kwa timu zitakazoshika nafasi mbili za juu kwenye kila kundi zitaingia hatua ya nusu fainali itakayochezwa Juni 30 na fainali imepangwa kucheza Julai 2.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICE ATAKIWA MAN

KLABU ya Manchester United imeungana na Arsenal kutika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa England, Declan Rice,24, kutoka West Ham, huku Mashetani Wekundu hao wakizingatia mkataba wa mchezaji pamoja na fedha inayomhusisha mlinzi wa England, Harry Maguire, 30, au kiungo wa Scotland, Scott McTominay, 26. ***(Telegraph)***

### TONALI KUTUA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inakaribia kufikia makubaliano ya pauni milioni 60 kumnunua kiungo wa AC Milan na Italia, Sandro Tonali, 23. ***(Athletic)***

### PHILLIPS ATAKIWA

MANCHESTER City inamyatia Declan Rice, huku West Ham wakipendelea dili ambalo lingemfanya kiungo wa England, Kalvin Phillips, 27, kuhamia kwao. ***(ESPN)***

### SILVA KWENDA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa Man City na Ureno, Bernardo Silva, 28, anakaribia kuhamia Saudi Arabia. ***(Marca)***

### BAYERN KUMUUZA MANE

KLABU ya Bayern Munich iko tayari kumuuza mshambuliaji wa Senegal, Sadio Mane, 31 msimu huu wa joto, huku Newcastle United ikimtaka. ***(Bild)***

### NEVES AWANIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United pia wanataka kumsajili Ruben Neves, 26, kwa mkopo baada ya kiungo huyo wa Ureno kukubali kujiunga na Al Hilal kutoka Wolverhampton kwa pauni milioni 47 wiki hii. ***(Football Insider)***

### KANE NA MAN U

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, 29, bado ana matumaini ya kuhamia Manchester United msimu huu wa joto. ***(Mirror)***

### SPURS YAMTAKA VICARIO

KLABU ya Tottenham Hotspur imekubali mkataba wa pauni milioni 17.2 kumsajili golikipa wa Italia, Guglielmo Vicario, 26, kutoka Empoli. (***Sky Sports)***

### MUANI ANYATIWA

MANCHESTER United na Bayern Munich zimepewa nafasi kubwa ya kumsajili mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt na Ufaransa, Randal Kolo Muani, 24. ***(L'Equipe)***

### ONANA ATAKIWA MAN

MANCHESTER United infikiria kumnunua kipa wa Inter Milan na Cameroon, Andre Onana, 27. ***(Sky Sports Italy)***

### O'SHEA AWANIWA BURNLEY

KLABU ya Burnley inatazamiwa kumsajili beki wa Jamhuri ya Ireland, Dara O'Shea, 24, kutoka West Bromwich Albion. ***(Irish independent)***

### KLUIVERT AWINDWA

BOURNEMOUTH inakaribia kukamilisha dili la pauni milioni 9.5 na AS Roma kwa ajili ya kumnunua mshambulizi wa Uholanzi, Justin Kluivert, 24. ***(Talksport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HAVERTZ ATUA RASMI ARSENAL

**LONDON,** England

ARSENAL wamekubali mkataba wenye thamani ya hadi pauni milioni 67.5 kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Kai Havertz, kwa mujibu wa ESPN.

**Mazungumzo yaliendelea haraka siku ya Jumatano kuhusu mkataba ambao Chelsea wamesema una thamani ya pauni 62.5 pamoja na pauni milioni 5 zaidi katika nyongeza zinazohusiana na kiwango cha uchezaji.**

Havertz anakuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa na kocha Mikel Arteta majira haya ya joto huku Washikabunduki hao wakitafuta pia kumsajili kiungo wa West Ham, Declan Rice na mlinzi wa Ajax, Jurrien Timber.

●●● Iliripoti Jumatatu kwamba alikuwa amewaarifu Blues hao kwamba hana nia ya...

ESPN iliripoti Jumatatu kwamba Havertz alikuwa amewaarifu Blues hao kwamba hana nia ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo.

Mkataba wake wa sasa ulikuwa unamalizika mwaka 2025 na Chelsea hawataki kuwa katika hali ambayo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 atapunguza mkataba wake, hivyo thamani yake iingeshuka.

Kocha mpya wa Chelsea, Mauricio Pochettino anataka kurekebisha fowadi yake msimu huu wa joto na ameamua kumruhusu Havertz kuondoka.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba wakati wa mazungumzo, Arsenal walibainisha kuwa pamoja na kuwa na uwezo wa kufanya kazi kama namba 10 au namba 8, wanaona Havertz kama chaguo linalowezekana katika mojawapo ya nafasi tatu za ushambuliaji katika safu ya mbele inayoweza kubadilishwa.

Havertz alifunga bao la ushindi katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2021, lakini alijitahidi kupata uthabiti katika uchezaji wake, akifunga mabao 32 katika michezo 139 katika mashindano yote.

# GUNDOGAN APEWA MIAKA MIWILI BARCA




**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imefikia makubaliano na Manchester City kumsajili Ilkay Gundogan kama mchezaji huru mkataba wake utakapokamilika Juni 30, kwa mujibu wa ESPN.

Gundogan mwenye umri wa miaka 32 amekubali mkataba wa miaka miwili na Barca huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja, akikataa ofa ya kuongeza muda wake wa kukaa City kwa misimu saba pamoja na mapendekezo kutoka kwa Arsenal na klabu za Saudi Arabia.

Masuala ya kifedha yanayoendelea ya Barcelona yalimaanisha walichunguza soko huria la mchezaji huru, na Machi ESPN ilifichua kuwa Barca walikuwa kwenye mazungumzo na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba City hawakutaka kufikia ofa ya kifedha ya Barca, na wangemuongeza tu mkataba wa mwaka mmoja.

Andreas Christensen na Franck Kessie wote waliwasili kwa uhamisho wa bure msimu uliopita wa joto, wakati vyanzo viliiambia ESPN kwamba mlinzi Inigo Martinez pia yuko tayari kujiunga na Barca baada ya kumalizika kwa mkataba wake na Athletic Club mwezi huu.

Gundogan anawasili Barca baada ya kocha Xavi Hernandez kueleza nia ya kuboresha ubunifu wa timu na idadi ya mabao kutoka katikati ya uwanja baada ya kumkosa Lionel Messi, ambaye atajiunga na Inter Miami.

Xavi alihisi Barca ilitatizika msimu uliopita Pedri alipoumia, na Gundogan anaonekana kama mtu anayeweza kusaidia.

Barca inathamini uwezo wa mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund katikati ya uwanja, haswa uwezo wake -- ingawa vyanzo vimesema klabu bado inggependelea kuleta mbadala wa moja kwa moja wa Sergio Busquets anayeondoka.

# Mourinho apigwa rungu na UEFA

**NYON,** Uswisi

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho amefungiwa mechi nne na Shirikisho la soka Ulaya, UEFA, kwa kosa la kumbwatukia mwamuzi kwenye fainali ya Ligi ya Europa mwezi uliopita.

Mreno huyo alikabiliwa na shutuma nyingi baada ya kumtusi mwamuzi wa England, Anthony Taylor kufuatia kufungwa kwa timu yake na Sevilla kwa mikwaju ya penalti.

UEFA pia ilitangaza kuwa mashabiki wa West Ham watapigwa marufuku kushiriki mechi yao ijayo ya ugenini katika mashindano ya Ulaya.

Hiyo ilihusiana na mashabiki wa Wagonga nyundo hao kurusha makombora uwanjani wakati wa ushindi wao wa fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Fiorentina mjini Prague mapema mwezi huu.

Beki wa klabu hiyo ya Italia, Cristiano Biraghi alijeruhiwa kichwani na kitu kilichorushwa kutoka kwa kwenye umati huo.

Mourinho alimkosoa Taylor katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi na, katika picha za video ambazo baadaye ziliibuka kwenye mitandao ya kijamii, kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Manchester United alionekana akimzonga Taylor na maafisa katika maegesho ya magari.





# Kovacic mali ya Manchester City

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imekubaliana na Chelsea kumnunua kiungo Mateo Kovacic, vyanzo viliiambia ESPN.

City wanatazamiwa kulipa pauni milioni 25 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia, huku pauni nyingine milioni 5 zikitakiwa kuongezwa baadae.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Chelsea walikuwa na matumaini ya kukubaliana mkataba wa karibu pauni milioni 35, lakini walipunguza matakwa yao ili kufikia makubaliano kabla ya Juni 30.

Malipo yatakayokamilika kabla ya hapo yatakuwa chini ya mwaka wa kwanza kamili wa ushuru na usaidizi na Chelsea inatii sheria za UEFA za haki sawa ya kifedha.

Kovacic atafanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kabla ya kujiunga na kikosi cha kocha Pep Guardiola kwa ajili ya ziara ya Man City ya kujiandaa na msimu mpya nchini Japan na Korea Kusini, itakayoanza mwishoni mwa Julai.

City wamehamia haraka kwa Kovacic ili kuimarisha safu yao ya kiungo baada ya kukosa dili la kumnunua Jude Bellingham, ambaye alijiunga na Real Madrid akitokea Borussia Dortmund.

Guardiola na mkurugenzi wa soka, Txiki Begiristain wameshindwa kumshawishi Ilkay Gundogan ambaye amefikia makubaliano ya kujiunga na Barcelona, huku pia kuna shaka kuhusu mustakabali wa Bernardo Silva pale Etihad.

Silva yuko chini ya mkataba hadi mwaka 2025 lakini anataka changamoto mpya baada ya miaka sita nchini England.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba ana nia ya kujiunga Barcelona na Paris Saint-Germain lakini City itadai ada kubwa kabla ya kumruhusu kuondoka.

Kulingana na vyanzo City pia wana nia ya kumnunua Declan Rice wa West Ham lakini bado hawajawasilisha ofa. Arsenal tayari wametoa ofa mbili kwa kiungo huyo wa kati wa Uingereza aliyepigwa tena.

HABARI MICHEZO

# YANGA YAKANUSHA LOMALISA KUONDOKA

Na Mwandishi Wetu

KLBU ya Yanga imekanusha kuwa beki wake wa pembeni Joyce Lomalisa anaondoka klabuni hapo baada ya kupeleka barua ya kuomba kuondoka.

**Uongozi wa klabu hiyo umesema mchezaji huyo haondoki klabuni hapo kwa kuwa wana mkataba naye wa mwaka mmoja zaidi na hakuna ofa yoyote ya kutaka kumsajili iliyowasilishwa klabuni hapo.**

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe amesema jana kuwa taarifa zinazosema kuwa mchezaji huyo ameomba kuondoka au anaondoka kwa sababu mkataba umemalizika si za kweli, hivyo kuwatoa hofu wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

"Kuna taarifa zinaanzishwa kwa ajili ya kutaka kuvuruga utulivu wetu, kwa mlengo wa kibiashara, au mawakala wanatengeneza tu ili wachezaji wao wajadiliwe kupata mikataba mikubwa zaidi, Lomalisa ni mchezaji wetu halali amebakisha mkataba wa mwaka mmoja, na kama hawa wachezaji wote wa Yanga wenye mikataba watataka kuondoka kwenye klabu yetu, maana yake ni lazima wafuate taratibu ambazo viongozi wa Yanga ni lazima wakae chini waziangalie ofa," alisema Kamwe.

Kamwe amewataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kuwa watulivu hasa kipindi hiki cha usajili ambapo watasikia mengi yanayowahusu wachezaji wo kwa sababu wamefanya vyema kwenye michuano ya kimataifa.

"Kwanza niwaambie wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa tupo kwenye kipindi cha usajili, kipindi hiki kina habari nyingi kweli kweli, kuna tetesi nyingi sana, muhimu ni kuamini tu yale ambayo viongozi wao tutayasema kupitia vyanzo rasmi vya klabu au kupitia mahojiano tunayoyafanya na vyombo vya habari wakisikia tunazungumza, Yanga ni klabu kubwa hivi sasa ndiyo maana wachezaji wetu kila siku wanahusishwa kuondoka kwenye klabu yetu," alisema Kamwe.

Wakati huo huo klabu hiyo imeachana na winga wake machachari, Bernard Morrison raia wa Ghana, baada ya kukaa kwa msimu mmoja.



Mchezaji wa timu ya Afya Kuu, Fadhili Issa (kulia), akiwania mpira na mchezaji wa timu ya vijana wanaolelewa katika kituo cha kukuza vipaji wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga: Tutatengeneza timu bora

INATOKA UKURASA 24

wote wenye mikataba na wanataka kuondoka kwenda timu nyingine wanatakiwa kusubiri hizo timu zipeleke ofa mezani kwao (Yanga) na kama watakubaliana nazo watawaruhusu kuondoka.

Kwa siku za karibu baada ya ligi kuisha, wachezaji Djuma Shaaban, Fiston Mayele, Joyce Lomalisa na Yanick Bangala wamehusishwa kutaka kuondoka klabuni hapo.

## Azam yaizidi kete Simba kwa Bajana

Na Adam Fungamwango

BAADA ya tetesi kuwa Simba ipo mbioni na ina matumaini ya kumsajili kiungo mkabaji Sospeter Bajana kutoka Azam, uwezekano huo sasa umefutwa rasmi baada ya nyota huyo kuongeza mkataba wa miaka mitatu kuendelea kusalia kwenye klabu yake.

Azam FC jana walitangaza kumpa mkataba wa miaka mitatu kiungo huyo baada ya kufikia makubaliano pande zote mbili.

Bajana ambaye alionyesha kiwango kikubwa msimu uliopita, alikuwa akiwaniwa na Simba baada ya mkataba wake wa awali kumalizika mwishoni mwa msimu uliopita.

Mchezaji huyo amesaini mkataba huo juzi jioni mbele ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC Abdulkarim Amin 'Popat' na kufuta uwezekano wa nyota huyo kutimkia Simba kama ilivyokuwa ikielezwa awali.

"Mkata umeme halisi na nahodha wetu Bajana, bado ataendelea kusalia kwenye viunga vya Azam Complex hadi mwaka 2026," ilisema taarifa ya klabu hiyo kwenye mtandao wake.

Baada ya kumwaga wino, mchezaji huyo ambaye alikuwa kwenye kiwango cha juu msimu huu, alisema msimu ujao ataipambania klabu hiyo ili iweze kutwaa mataji.

"Ni furaha kubwa ni timu ya moyoni mwangu, naipenda sana na niko tayari kuipigania kwa jasho na damu kuhakikisha tunaleta tena mataji nyumbani," alisema mchezaji huyo.

Azam imeonekana kutaka kujidhatiti kuelekea msimu ujao wa ligi, kwani pamoja na kumbakisha Bajana, imemsajili kiungo mshambuliaji Feisal Salum kutoka Yanga, huku ikiachana na baadhi ya watu wa benchi lao la ufundi na wachezaji kadhaa wakiwemo Mzambia Rodgars Kola, Mkenya Kenneth Muguna, Mzimbabwe Bruce Kangwa na wazawa Cleophace Mkandala, Ismail Kada na Wilbol Maseke.

## Kakolanya aaga

INATOKA UKURASA 24

kwamba mkataba umeisha baada ya ligi kumalizika," alisema Kakolanya.

Akizungumzia kutopangwa kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa akiwa kama kipa namba mbili, badala yake kipa namba tatu alikuwa anachukua nafasi yake, Beno alisema ilikuwa ni hali tu ya mchezo na kwamba hata yeye ilishawahi kumtokea huko nyuma akiwa kwenye kikosi cha Prisons ambapo alianza kuicheza timu hiyo akiwa golikipa namba tatu.

Kwa upande wake, Nyoni aliyejiunga na Simba mwaka 2017 akitokea Azam FC amepewa mkono wa kwa heri na uongozi wa timu hiyo.

"Uongozi wa klabu unautangazia umma kuwa hatutaendelea kuwa na mchezaji wetu kiraka Erasto Nyoni baada ya mkataba wake kumalizika," ilisema sehemu ya taarifa ya klabu hiyo.

Nyoni alianza kuchipukia akiwa kwenye kituo cha soka cha Rolling Stone cha Jijini Arusha, baadae alijiunga na klabu ya AFC ya Jijini humo kabla ya kwenda kucheza soka la kulipwa nchini Burundi kwenye klabu ya Vital'O mwaka 2009 na mwaka mmoja baadaye akasajiliwa na Azam FC.

# Michezo

Ijumaa Juni 23, 2023
Nipashe



Gundogan apewa miaka miwili Barca

UKURASA 22

# 'Tutajenga timu bora kwa gharama yoyote'



●●● Rais Hersi awataka wanachama kusubiri furaha, awaita kwenye....

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umesema utatumia gharama yoyote kuandaa timu bora kwa ajili ya msimu ujao na wataruhusu wachezaji wao bora kuondoka kikosini kwao na kuwataka mashabiki wasubiri furaha nyingine.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Rais wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said, alisema kumekuwepo na tetesi nyingi katika kipindi hiki cha usajili lakini uongozi wake upo makini na watakuwa na kikosi bora msimu ujao.**

Alisema Wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wawe watulivu na muda utakapowadia watashangaa na kufurahi aina ya kikosi watakachokuwa nacho kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano.

"Uongozi tupo makini na tunajua nini tunachofanya, tulikuwa na msimu mzuri, msimu ujao tutakuwa na kikosi bora zaidi, tutatumia gharama yoyote kuhakikisha hili linafanikiwa na kuendelea kufanya vizuri, alisema Hersi na kuendelea,

"Bado tuko katika mabadiliko na haitoshi bado tunaendelea kujenga timu kwa gharama yoyote ile ili Yanga iwe imara leo na kesho, Wanayanga wote nawaomba muwe watulivu muda wetu utakapofika kila mtu atafurahi tumejipanga vyema sana," alisema Hersi.

Alisema mipango yao wataigusia kwenye mkutano wao mkuu wa kesho na kuwataka wanachama wenye sifa wanaotakiwa kushiriki mkutano huo kujitokeza kwa wingi.

"Niwaombe wanachama wa Yanga tuendelee kuwa na ushirikiano tuijenge Yanga yetu ili iweze kufikia mafanikio makubwa na kuifanya kuwa klabu kubwa Afrika" alisema Hersi.

Alisema kwa mujibu wa ibara 17 (1) ya Katiba ya Yanga wanaotakiwa kuhudhuria Mkutano Mkuu ni Mwenyekiti wa tawi, Katibu wa tawi, Mweka hazina na wajumbe wawili wa Mkutano Mkuu kutoka kwenye tawi.

Aliongeza kuwa katika mkutano huo wataeleza mambo mbalimbali ikiwemo tathimini ya timu yao kwa msimu wa 2022/23 uliomalizika hivi karibuni pamoja na mipango yao ya msimu ujao katika kuimarisha kikosi cha timu hiyo.

Pia alisema wataelezea mipango yao kwa wachezaji wao waliopo kwenye kikosi chao kilichofanya vizuri msimu uliopita.

Alisema kumekuwa na taarifa nyingi zinazowahusu baadhi ya wachezaji wao kuhusishwa kutaka kuondoka klabuni hapo.

Alisema wachezaji wote wanaohusishwa kuondoka bado wana mikataba nao na ni mali ya halali.

"Yanazungumzwa mengi, lakini niwahakikishie wanayanga wachezaji wanozungumzwa sana kuwa wanataka kuondoka, wote wana mikataba na klabu," alisema Hersi.

Aidha, alisema wachezaji

INAENDELEA UKURASA 23

# Kakolanya aaga Simba, Nyoni naye kwaheri

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA namba mbili wa klabu ya Simba, Beno Kakolanya ameaga rasmi ndani ya klabu hiyo na hataitumikia tena msimu ujao baada ya kumaliza mkataba wake.

Wakati Kakolanya akiaga na kuondoka ndani ya timu hiyo, Simba jana jioni imetangaza kuachana na kiungo wake mkongwe Erasto Nyoni aliyedumu ndani kikosi hicho kwa miaka sita.

Akizungumza jana Jijini Dar es Salaam, Beno amesema aliipa nafasi ya kwanza Simba lakini hawakufikia dau walilokubaliana na zikaja ofa mbili kutoka Uarabuni na hapa nchini lakini la hapa nchini likawa nono zaidi.

"Mpira ni mchezo wa muda mfupi sana ni lazima ucheze kwa malengo, mimi nimemaliza mkataba na Simba sasa ni mchezaji huru, lakini kabla ya hapo niliipa nafasi timu yangu lakini ofa yao ilikuwa ndogo, ikaja klabu kutoka Uarabuni wakapanda dau, ghafla ikaja nyingine kutoka hapa hapa, wenyewe wakatoa dau nono zaidi," alisema Kakolanya.

Kakolanya anahusishwa kuwa ameshamalizana na klabu ya Singida Fountain Gate na alikuwa anasubiri mkataba wake kuisha Simba ili ajiunge nayo rasmi.

Aidha, Kakolanya aliyejiunga na Simba mwaka 2019, amekanusha taarifa kuwa alikuwa hachezi mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa sababu mkataba ulikuwa umemalizika.

"Haikuwa kweli kwamba nilikuwa sichezi kwa sababu mkataba ulikuwa umemalizika yaani kama ungekuwa umekwisha hata mazoezi nisingecheza, achilia mbali kukaa benchi, mechi zote mimi nilikaa benchini, haiwezekani uwe umemaliza mkataba halafu ufanye hivyo, ukweli ni

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042